**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

## WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM




# TAARIFA YA MCHANGO WA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI KATIKA MAENDELEO YA TAIFA KWA MWAKA 2024

**Agosti, 2025**

## YALIYOMO

YALIYOMO ..... i
VIFUPISHO ..... v
ORODHA YA MAJEDWALI ..... vi
ORODHA YA MAUMBO ..... vii
DIBAJI ..... viii
SHUKRANI ..... x
MUHTASARI WA TAARIFA ..... xii
SURA YA KWANZA ..... 1
MSINGI, MALENGO NA WALENGWA TAARIFA YA MCHANGO ..... 1
WA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI ..... 1
1.1 Utangulizi ..... 1
1.2 Msingi wa Taarifa ..... 2
1.3 Malengo ya Taarifa ..... 2
1.4 Walengwa wa Taarifa ..... 3
1.5 Mawanda ya Uchambuzi ..... 3
1.6 Mbinu Zilizotumika ..... 3
SURA YA PILI ..... 4
USAJILI NA URATIBU WA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI ..... 4
KWA UPANDE WA TANZANIA BARA ..... 4
2.1 Utangulizi ..... 4
2.2 Usajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ..... 4
2.3 Mahitaji ya Kisheria na Kikanuni Baada ya Usajili ..... 6
2.4 Uwasilishaji wa Taarifa na Ulipaji wa Ada ..... 7
SURA YA TATU ..... 10
UIMARISHAJI WA MAZINGIRA WEZESHI YA UTENDAJI KAZI ..... 10
WA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI ..... 10

3.1 Utangulizi ........ 10
3.2 Mwongozo wa Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ........ 10
3.3 Mkakati wa Uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ........ 11
3.4 Mfumo wa Kielektroniki wa Usajili na Uratibu wa Mashirika ........ 11
3.5 Madawati ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ........ 12
3.6 Majukwaa ya Mwaka ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ........ 13
3.7 Vikao Kazi vya Kisekta kati ya Wizara na Mashirika ........ 14
3.8 Ziara za Kujifunza na Kubadilishana Uzoefu wa Uratibu ........ 14
SURA YA NNE ........ 16
VYANZO VYA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA ZA MASHIRIKA ........ 16
YASIYO YA KISERIKALI ........ 16
4.1 Utangulizi ........ 16
4.2 Mapato ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ........ 16
4.3 Matumizi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ........ 18
SURA YA TANO ........ 20
MCHANGO WA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI KATIKA ........ 20
NYANJA MBALIMBALI ZA MAENDELEO ........ 20
5.1 Utangulizi ........ 20
5.2 Utekelezaji wa Miradi na Afua Kisekta ........ 20
5.2.1 Uwezeshaji wa Jamii ........ 22
5.2.2 Sekta ya Afya ........ 23
5.2.3 Uhifadhi wa Mazingira ........ 23
5.2.4 Sekta ya Elimu ........ 24
5.2.5 Ulinzi wa Jamii ........ 25
5.2.6 Sekta ya Kilimo ........ 27

5.2.7 Utawala Bora ..... 28
5.2.8 Sekta ya Maji ..... 29
5.2.9 Haki za Binadamu ..... 30
5.2.10 Masuala ya Kijinsia ..... 31
5.3 Wanufaika wa Miradi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ..... 32
5.4 Ajira Zilizozalishwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ..... 34
5.5 Makato ya Kisheria ya Posho na Mishahara ya Waajiriwa ..... 35
SURA YA SITA ..... 37
UTEKELEZAJI WA MKAKATI WA KITAIFA WA UENDELEVU WA ..... 37
MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI ..... 37
6.1 Utangulizi ..... 37
6.2 Malengo ..... 37
6.3 Utekelezaji na Fursa Zilizopo ..... 38
6.4 Tathmini ya Utekelezaji wa Mkakati ..... 38
6.5 Mafanikio ya Utekelezaji wa Mkakati ..... 38
6.5.1 Umiliki wa Majengo na Miundombinu ..... 39
6.5.2 Uanzishaji wa Taasisi za Kifedha ..... 41
6.5.3 Uwekezaji katika Kilimo na Ufugaji ..... 41
6.5.4 Miradi Mingine ya Kiubunifu na Kijamii ..... 42
6.6 Changamoto za Utekelezaji wa Mkakati ..... 43
6.7 Mapendekezo ..... 44
SURA YA SABA ..... 45
MWENENDO WA UFADHILI KWA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI KATIKA KIPINDI CHA MIAKA MITANO ILIYOPITA ..... 45
7.1 Utangulizi ..... 45

7.2 Mwenendo wa Ufadhili kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ........................ 45
7.2.1 Vyanzo vya Mapato na Matumizi ya Mashirika ........................................ 46
7.3 Utekelezaji wa Miradi na Afua Kisekta ....................................................... 50
7.4 Wafadhili wa Miradi na Afua za Mashirika .................................................. 54
7.5 Tathmini ya Jumla ....................................................................................... 57
SURA YA NANE ....................................................................................................... 58
CHANGAMOTO NA MAPENDEKEZO YA KUBORESHA URATIBU ................................ 58
WA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI ..................................................................... 58
8.1 Utangulizi ...................................................................................................... 58
8.2 Changamoto .................................................................................................. 58
8.3 Mapendekezo ................................................................................................ 59
8.4 Hitimisho ....................................................................................................... 61
REJEA ....................................................................................................................... 62

# VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| AWF | African Wildlife Foundation |
| BOT | Bank of Tanzania |
| CDC | Centre for Disease Control |
| CIC | Chilldren in Crossfire |
| DRC | Danish Refugee Council |
| EU | European Union |
| FCDO | Foreign, Commonwealth and Development Office |
| GAC | Global Affairs Canada |
| GePG | Government Electronic Payment Gateway |
| GFFO | German Federal Foreign Office |
| JMT | Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| KOICA | Korean International Cooperation Agency |
| NaCoNGO | National Council of Non-governmental Organizations |
| NIDA | National Identification Authority |
| NIS | NGOs Information System |
| NORAD | Norwegian Agency for Development Cooperation |
| NSSF | National Social Security Fund |
| OR-TAMISEMI | Ofisi ya Rais – Tawala za Mikao na Serikali za Mitaa |
| OSPC | Open Society Policy Centre |
| PAYE | Pay As You Earn |
| PEPFAR | President's Emergency Plan for Aids Relief |
| SDL | Skills Development Levy |
| SIDA | Swedish International Development Cooperation Agency |
| UNFPA | United National Population Funds |
| UNHCR | United Nations High Commission for Refugees |
| UNICEF | United Nations Children's Fund |
| USAID | United Nations Agency for International Development |
| WCF | Workers Compensation Fund |
| WWF | World Wide Fund for Nature |

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 2.2.1: Usajili wa Mashirika kwa Mwaka 2024……..............................5
Jedwali 2.2.2: Usajili wa Mashirika Kufikia Desemba 2024..................5
Jedwali 2.4.1: Mashirika Yaliyolipa Ada na Kuwasilisha Taarifa.............7
Jedwali 2.4.2: Idadi ya Mikataba Iliyowasilishwa na Kuidhinishwa.........8
Jedwali 4.2: Vyanzo vya Mapato ya Mashirika................................16
Jedwali 4.3: Matumizi ya Fedha za Mashirika...............................18
Jedwali 5.2: Idadi ya Miradi na Fedha Zilizotumika Kisekta.....................21
Jedwali 5.3: Idadi ya Waliofikiwa na Miradi Mbalimbali...........................33
Jedwali 5.4.1: Mgawanyo na Idadi ya Waajiriwa.........................................34
Jedwali 6.5.1: Umiliki wa Majengo na Miundombinu................................39
Jedwali 6.5.2: Uanzishaji wa Taasisi za Kifedha......................................41
Jedwali 6.5.3: Uwekezai Katika Ardha na Kilimo......................................41
Jedwali 6.5.4: Miradi Mingine ya Kiubunifu na Kijamii...............................42
Jedwali 7.2.1: Vyanzo vya Mapato ya Mashirika kwa Mwaka 2021..........47
Jedwali 7.2.2: Vyanzo vya Mapato ya Mashirika kwa Mwaka 2022..........47
Jedwali 7.2.3: Matumizi ya Fedha za Mashirika kwa Mwaka 2022.........48
Jedwali 7.2.4: Vyanzo vya Mapato ya Mashirika kwa Mwaka 2023..........48
Jedwali 7.2.5: Matumizi ya Fedha za Mashirika kwa Mwaka 2023.........49
Jedwali 7.2.6: Vyanzo vya Mapato ya Mashirika kwa Mwaka 2024..........50
Jedwali 7.2.7: Matumizi ya Fedha za Mashirika kwa Mwaka 2024.........50
Jedwali 7.3.1: Utekelezaji wa Miradi kwa Mwaka 2020.....................51
Jedwali 7.3.2: Utekelezaji wa Miradi kwa Mwaka 2021.....................51
Jedwali 7.3.3: Utekelezaji wa Miradi kwa Mwaka 2022.....................52
Jedwali 7.3.4: Utekelezaji wa Miradi kwa Mwaka 2023.....................53
Jedwali 7.3.5: Utekelezaji wa Miradi kwa Mwaka 2024.....................53
Jedwali 7.4.1: Wafadhili wa Miradi ya Mashirika Kisekta.....................54

## ORODHA YA MAUMBO


Umbo 2.2.1: Usajili wa Mashirika kwa Mwaka 2024............................5
Umbo 2.2.2: Usajili wa Mashirika Kufikia Desemba 2024.......................6
Umbo 2.4.1: Mashirika Yaliyolipa Ada na Kuwasilisha Taarifa..................8
Umbo 2.4.2: Asilimia ya Mikataba Iliyowasilishwa na Kuidhinishwa.........9
Umbo 4.2: Vyanzo vya Mapato ya Mashirika..................................17
Umbo 4.3: Matumizi ya Fedha za Mashirika.................................18
Umbo 5.2: Asilimia ya Fedha Zilizotumika katika Miradi Kisekta….........21
Umbo 5.3: Asilimia ya Waliofikiwa na Miradi………...........................…........33
Umbo 5.4.1: Mgawanyo na Idadi ya Waajiriwa……………........……………...34
Umbo 5.4.2: Mgawanyo wa Ajira kwa Jinsia……………….........…………………35
Umbo 7.2.1: Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2020...........................46

# DIBAJI

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kupitia Ofisi ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ina jukumu la kusajili na kuratibu Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali unatekelezwa kwa kuzingatia matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2001 na Sheria ya Mashirika ya Kiserikali, Sura ya 56 ya Sheria za Tanzania.

Kama mnavyofahamu, Sekta ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali imeendelea kukua kwa kasi kutoka Mashirika 2,110 mwaka 2005 hadi Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 10,120 kufikia mwezi Desemba 2024. Ni matarajio ya Wizara yenye dhamana ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yataendelea kutekeleza shughuli zake kwa kuzingatia misingi ya uwazi na uwajibikaji kama ilivyoainishwa katika sera, sheria, sanuni na miongozo ya uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Tanzania Bara.

Kama sehemu ya jitihada za Serikali katika kuongeza utambuzi wa mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika nyanja mbalimbali, Wizara imeandaa Taarifa ya Mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Maendeleo ya Taifa kwa mwaka 2024, ambapo pamoja na mambo mengine, imeainisha mchango wa Mashirika hayo katika utekelezaji wa miradi na afua katika sekta ya uwezeshaji wa jamii, afya, mazingira, elimu, ulinzi wa jamii, kilimo, utawala bora, maji, haki za binadamu, jinsia, nishati na miundombinu na viwanda.

Miradi na afua zilizotekelezwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Desemba 2024, sio tu zimewanufaisha wananchi wa Tanzania kupitia uboreshaji wa miundombinu, kilimo, mazingira na viwanda, bali pia zimechangia katika kuboresha utoaji wa huduma za kijamii, kuongeza fursa za ajira hasa kwa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu, pamoja na kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi wa mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla.

Aidha, katika kuhakikisha kuwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanaendelea kutoa mchango wake katika maendeleo ya Taifa, Serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi ya utendaji kazi, ikiwemo kuimarisha Mfumo wa Kielektroniki wa Usajili na Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa kuongeza Ramani ya Kidigitali ya Utambuzi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, ambayo ni nyenzo muhimu itakayosaidia kutambua mahali yalipo Mashirika, pamoja na miradi na afua zinazotekelezwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kupitia teknolojia rahisi ya kiganjani.

Masuala mengine ni kuendelea kuandaa Kitabu cha Mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Maendeleo ya Taifa, kuimarisha Madawati ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Wizara, Taasisi za Serikali na Sekta Binafsi, kuratibu Majukwaa ya Mwaka na Vikao Kazi vya Kisekta, pamoja na kusimamia utekelezai wa Mkakati wa Kitaifa wa Uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (2022/23–2026/27), ambao ulizinduliwa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), tarehe 04 Oktoba, 2022 ikiwa ni utekelezaji wa maelekezo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ***Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan***, aliyoyatoa tarehe 30 Septemba, 2021 wakati wa Kilele cha Jukwaa la Mwaka la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

Kwa kuzingatia umuhimu na mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika nyanja mbalimbali, napenda kutoa wito kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuendelea kutekeleza shughuli zao kwa kuzingatia misingi ya uwazi na uwajibikaji, kuimarisha ushirikiano wa kiutendaji baina yake na wadau wengine wa maendeleo, pamoja na kuhakikisha kunakuwepo na uendelevu wa Mashirika hayo hapa nchini. Ni matumaini yangu kuwa taarifa hii itakuwa chachu kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na wadau wengine wa kuendelea kutekeleza shughuli zao kwa uwazi na uwajibikaji.

Dkt. John A.K. Jingu
**KATIBU MKUU**
**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM**

## SHUKRANI

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum inapenda kutoa shukrani za pekee kwa watu na taasisi mbalimbali ambazo kwa namna moja au nyingine zimeshiriki katika mchakato wa upatikanaji wa rasilimali fedha, uwezeshaji, uandaaji, uhariri, usanifu, uchapishaji na usambazaji wa Kitabu cha Mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Maendeleo ya Taifa kwa mwaka 2024.

Shukrani za dhati ziende kwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mhe. Dkt. Dorothy Gwajima (Mb); Katibu Mkuu, Dkt. John Jingu; Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Maendeleo ya Jamii na Makundi Maalum, Wakili Amon Mpanju; na Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Jinsia na Wanawake, Bi. Felister Mdemu, kwa kuiwezesha Ofisi ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutekeleza jukumu lake na msingi la kusajili na kuratibu shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa weledi na ufanisi wa hali ya juu.

Vilevile, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Bodi ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali chini ya Mwenyekiti wake, Hajjat Mwantumu Mahiza, kwa usimamizi na uratibu uliotukuka wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa upande wa Tanzania Bara. Aidha, shukrani ziende kwa Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO) chini ya Mwenyekiti wake Bw. Jasper Makala na Katibu Mkuu wake Bw. Adamson Nsimba, kwa ushirikiano thabiti ambao wamekuwa wakiutoa kwa Wizara na Serikali kwa ujumla katika kuratibu na kusimamia sekta ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa upande wa Tanzania Bara.

Vilevile, shukrani ziende kwa Menejimenti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa michango yao iliyowezesha uboreshaji wa fani na maudhui ya Kitabu cha Mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Maendeleo ya Taifa kwa mwaka 2024. Ninawashukuru pia kwa maoni mliyoyatoa na kuridhia kwenu kuchapishwa kwa Kitabu hiki ili kiweze kutumiwa sio tu Mashirika Yasiyo ya Kiserikali,

bali pia na Washirika wa Maendeleo, Sekta Binafsi, Wanufaika wa Miradi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na jamii ya Watanzania kwa ujumla.

Aidha, napenda kutumia fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Timu ya Wataalam iliyopewa jukumu la kuratibu uandaaji wa Kitabu cha Mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Maendeleo ya Taifa kwa mwaka 2024, wakiongozwa na Bw. Charles Komba (Mwenyekiti), Bw. Abraham Mushashu (Katibu) na Bi. Francisca Ngw'endesha (Mratibu). Wajumbe wengine ni Bi. Josephine Mchalange, Bw. Dennis Bashaka, Bw. Issa Mtinangi, Bi. Modesta Komba na Bw. Jacob Melubo. Ninawashukuru sana kwa kazi nzuri mliyoifanya!

Mwisho, lakini sio kwa umuhimu, napenda kutoa shukrani za kipekee kwa Kampuni ya *Speedy Print Limited*, Shirika la *The Creator Share Foundation*, Shirika la *Aqua Farms Organization*, Shirika la *PELUM Tanzania*, Shirika la *Australian Volunteers International*, Shirika la *Hand in Hand*, Shirika la *Room to Read*, Shirika la *Juza Waste Pickers Initiative (JWPI)*, Shirika la *Tanzania Human Rights Coalition (THRDC), Norwegian Church Aid (NCA)* na Shirika la *AIDS Healthcare Foundation (AHF)* kwa kuwezesha uchambuzi, uandaaji, uhariri, usanifu na uchapishaji wa nakala za Kitabu cha Mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa Mwaka 2024.

Vickness G. Mayao
**MSAJILI WA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI**
**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM**

# MUHTASARI WA TAARIFA

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ni miongoni mwa wadau muhimu wa katika jitihada za Serikali kuwaletea wananchi maendeleo na kuimarisha ustawi wa jamii na Taifa kwa ujumla. Kwa upande wa Tanzania Bara, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kupitia Ofisi ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ina jukumu la kuratibu Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa mujibu wa Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo inayosimamia Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

Kufuatia hali hiyo, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imekuwa ikiandaa taarifa ya mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, ikiwa ni sehemu ya nyenzo muhimu ya kupima utendaji kazi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika mwaka husika. Hivyo, Taarifa ya Mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Maendeleo ya Taifa kwa mwaka 2024 imegawanyika katika sura saba, ambapo Sura ya Kwanza imeelezea msingi na malengo ya kuandaliwa kwa taarifa hii, walengwa wa taarifa, mawanda na mbinu zilizotumika katika uandaaji wa taarifa hii.

Sura ya Pili imeelezea usajili na uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa kubainisha mfumo wa kisheria wa uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, ikiwa ni hali ya usajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, mahitaji ya kisheria na kikanuni baada ya usajili, pamoja na hali ya ulipaji wa ada na uwasilishaji wa taarifa, zikiwemo za mikataba ya ufadhili.

Sura ya Tatu imeelezea mikakati mbalimbali iliyochukuliwa na Serikali katika kuimarisha mazingira wezeshi kwa utendaji kazi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, ikiwa ni pamoja na Mwongozo wa Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Tanzania Bara, Mfumo wa Kielektroniki wa Usajili na Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Mkakati wa Kitaifa wa Uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Madawati ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Majukwaa ya Mwaka ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, vikao kazi vya kisekta kati ya Wizara na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, pamoja na ziara za kujifunza na kubadilishana uzoefu.

Sura ya Nne ya taarifa hii imeelezea vyanzo vya mapato, matumizi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, ambapo kupitia uchambuzi wa taarifa za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 1,360, imebainika kuwa kiasi cha Shilingi 1,449,748,642,857 kilipokelewa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na kwamba kiasi cha Shilingi 1,289,344,177,596 kilitumika kwa ajili ya utekelezaji wa miradi na shughuli mbalimbali za kiutawala.

Sura ya Tano ya taarifa hii imejikita kuelezea mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika nyanja mbalimbali, ambapo sekta iliyoongoza kwa mwaka 2024 ilikuwa ni sekta ya uwezeshaji wa jamii, ikifuatiwa na sekta ya afya, mazingira, elimu, ulinzi wa jamii, kilimo, utawala bora, maji, haki za binadamu, jinsia, nishati, miundombinu na viwanda.

Sura hiyo pia imeelezea kwa kina kuhusu makundi yaliyonufaika zaidi na miradi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, ambapo vijana walifikiwa zaidi kwa asilimia 42, wakifuatiwa na wanawake asilimia 23, wazee asilimia 11 na watoto asilimia 09. Aidha, jumla ya Watanzania 12,272 na raia wa kigeni 131 walikuwa wameajiriwa, wakati Watanzania 5,761 na raia wa kigeni 365 walikuwa wanafanya kazi za kujitolea katika Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika kipindi cha Mwezi Januari hadi Desemba, 2024.

Sura ya Sita imetoa maelezo kuhusu hatua mbalimbali za utekelezaji wa *Mkakati wa Kitaifa wa Uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali* (2022/23–2026/27) uliozinduliwa mwaka 2022. Mkakati huo unalenga kusaidia Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kujitegemea kifedha, kuboresha uwezo wao wa kitaasisi na kuimarisha ushirikiano wa kimkakati kwa maendeleo ya muda mrefu. Katika mwaka husika, utekelezaji wa Mkakati ulibainika katika umiliki wa majengo na miundombinu, uanzishaji wa taasisi za kifedha, uwekezaji katika kilimo na ufugaji, uwekezaji katika ardhi na kilimo, pamoja na miradi mingine ya kiubunifu na kijamii.

Sura ya Saba imeelezea mwenendo wa ufadhili kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2020–2024), hususan kwa kufanya uchambuzi wa vyanzo vya mapato na matumizi ya fedha za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kupitia utekelezaji wa miradi na afua katika

sekta mbalimbali, pamoja na wafadhili wakuu wa miradi na afua za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika kipindi cha miaka mitano.

Sura ya Nane imejikita kuelezea changamoto mbalimbali katika uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, ikiwemo changamoto ya upatikanaji wa rasilimali fedha na baadhi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutowasilisha taarifa na wengine kushindwa kutumia Mfumo wa NIS. Baadhi ya mapendekezo yaliyotolewa ni pamoja na kuendelea kuyajengea uwezo Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuhusu matumizi ya Mfumo wa NIS kwa aili ya uwasilishaji wa taarifa na kuimarisha mazingira wezeshi kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

# SURA YA KWANZA

## MSINGI, MALENGO NA WALENGWA TAARIFA YA MCHANGO WA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI

### 1.1 Utangulizi

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kupitia Ofisi ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ina jukumu la kusajili na kuratibu Mashirika Yasiyo ya Kiserikali nchini kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sura ya 56 ya Sheria za Tanzania. Aidha, Sera ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2001 imeweka misingi ya uwazi na uwajibikaji kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali pamoja na kuhimiza ubia kati ya Serikali na Mashirika hayo ili kutambua mchango wao kwa jamii.

Katika kutekeleza hilo, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali hutakiwa kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa kazi wanazofanya katika kipindi cha robo mwaka na mwaka ili kuwezesha utambuzi wa shughuli zilizotekelezwa pamoja na mchango wake katika maendeleo ya Taifa. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Wizara ya Fedha, Wizara, Idara na Taasisi za Kisketa, pamoja na Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zimekuwa zikifanya ufuatiliaji na tathmini ya shughuli au miradi inayotekelezwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

Kupitia ufuatiliji huo, Serikali na wadau mbalimbali hupata fursa ya kutathmini mchango unaotolewa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika maendeleo ya Taifa, pamoja na tija ya miradi inayotekelezwa na Mashirika hayo kwa jamii kwa kuzingatia sera, malengo na vipaumbele mbalimbali vya Taifa. Aidha, ufuatiliaji na tathmini ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali hujikita kupima mwenendo wa utekelezaji wa majukumu ya Mashirika hayo kwa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo inayosimamia sekta hiyo, ikiwemo kubainisha mafanikio na changamoto za kiutendaji katika Sekta ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali hapa nchini.

## 1.2 Msingi wa Taarifa

Katika kipindi cha miaka ya hivi karibuni, kumekuwepo na uhitaji wa taarifa sahihi za mchango wa sekta ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutoka miongoni mwa wadau mbalimbali, zikiwemo Wizara, Idara na Taasisi za Serikali, Washirika wa Maendeleo, Sekta Binafsi, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi za Utafiti, Vyombo vya Habari, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na jamii kwa ujumla.

Kufuatia hali hiyo, Kitabu cha Taarifa ya Mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Maendeleo ya Taifa kilizinduliwa rasmi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ***Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan***, tarehe 30 Septemba, 2021 wakati wa kilele cha Jukwaa la Mwaka la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kilichofanyika Jijini Dodoma, ambapo alielekeza kazi ya uandaaji wa taarifa hiyo kuwa endelevu ili kuongeza utambuzi wa mchango wa Mashirika hayo katika nyanja mbalimbali.

## 1.3 Malengo ya Taarifa

Lengo kuu la uandaaji wa taarifa hii ni kutathmini ukuaji wa sekta na kupata picha halisi ya mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika maendeleo ya Taifa kupitia taarifa za utekelezaji wa miradi na afua zilizowasilishwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Desemba 2024. Malengo Mahsusi ni pamoja na:

- Kutambua kiwango cha rasilimali fedha kilichopokelewa na kutumiwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika utekelezaji wa miradi na afua mbalimbali.
- Kutambua idadi na aina ya miradi na afua zilizotekelezwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Desemba 2024.
- Kutambua idadi na makundi ya wanufaika wa miradi na afua mbalimbali zilizotekelezwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Desemba 2024.
- Kutathmini utelekezaji wa sera na mikakati mbalimbali, ikiwemo *Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22-*

*2025/26 na Mkakati wa Kitaifa wa Uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (2022/23-2026/27).*

- Kubainisha fursa na changamoto katika uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, hatua zinazochukuliwa na Wizara, Idara na Taasisi za Serikali, pamoja na Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiseriklai, na kutoa mapendekezo kwa wadau mbalimbali.

## 1.4 Walengwa wa Taarifa

Walengwa wa taarifa hii ni Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, ambayo ni Wizara yenye dhamana ya uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, pamoja na Wizara, Idara na Taasisi za Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, Washirika wa Maendeleo, Sekta Binafsi, Taasisi za Utafiti, Vyombo vya Habari, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na jamii kwa ujumla.

## 1.5 Mawanda ya Uchambuzi

Uchambuzi huu umehusisha taarifa za utekelezaji na taarifa za fedha zilizokaguliwa ambazo ziliwasilishwa kwa ukamilifu na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 1,360 kupitia Mfumo wa Kielektroniki wa Usajili na Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NIS), pamoja na taarifa za ufuatiliaji na tathmini ya miradi na afua zilizotekelezwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Mikoa 26 ya Tanzania Bara.

## 1.6 Mbinu Zilizotumika

Mbinu zilizotumika katika uandaaji wa taarifa hii ni pamoja na uchambuzi wa taarifa za utekelezaji na taarifa za fedha zilizokaguliwa, taarifa za robo mwaka na taarifa za mikataba ya ufadhili zilizowasilishwa na Mashirika katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Desemba 2024, taarifa za ufuatiliaji na tathmini, pamoja na mahojiano na viongozi, wafanyakazi na wanufaika wa miradi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

# SURA YA PILI

# USAJILI NA URATIBU WA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI KWA UPANDE WA TANZANIA BARA

## 2.1 Utangulizi

Kwa upande wa Tanzania Bara, usajili na uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali unafanyika kwa kuzingatia matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, ambapo imetoa haki kwa wananchi kujumuika katika makundi mbalimbali, pamoja na Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2001 na Sheria ya Mashirika ya Kiserikali, Sura ya 56 ya Sheria za Tanzania.

Aidha, Kifungu cha 31(a) na (b) cha Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sura ya 56 kinayataka Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutekeleza shughuli zao kwa kuzingatia sheria nyingine za Nchi, ikiwemo sheria za kodi, sheria za kazi na ajira, sheria za uhamiaji, sheria za kuzuia usafirishaji haramu wa binadamu, sheria za kupambana na ugaidi na utakasishaji wa fedha haramu, pamoja na uzingatiaji wa mila, desturi na utamaduni wa jamii inayowahudumia, hasa ukizingatia kuwa mila na tamaduni hizo hazikinzani na Sheria nyingine za Nchi.


## 2.2 Usajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali

Katika kipindi cha mwezi Januari hadi Desemba 2024, Wizara kupitia Ofisi ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali imeendelea kutekeleza majukumu yake ya kusajili Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, ambapo katika kipindi hicho, jumla ya Mashirika 1,439 yalisajiliwa katika ngazi mbalimbali; Kitaifa (1,318), Kimataifa (56), Kimkoa (39) na Kiwilaya (26). Hivyo, jumla ya Mashirika 10,120 yalikuwa yamesajiliwa kufikia mwishoni mwa mwaka 2024, kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali 2.2.1, Umbo 2.2.1, Jedwali 2.2.2 Umbo 2.2.2 hapo chini:

**Jedwali 2.2.1: Usajili wa Mashirika kwa Mwaka 2024**

| Na. | Ngazi za Usajili | Idadi ya Mashirika |
|---|---|---|
| 1. | Kiwilaya | 26 |
| 2. | Kimkoa | 39 |
| 3. | Kitaifa | 1,318 |
| 4. | Kimataifa | 56 |
| | **Jumla** | **1,439** |


**Umbo 2.2.1: Usajili wa Mashirika kwa Mwaka 2024**




**Jedwali 2.2.2: Usajili wa Mashirika Kufikia Desemba, 2024**

| Na. | Ngazi za Usajili | Idadi ya Mashirika |
|---|---|---|
| 1. | Kiwilaya | 542 |
| 2. | Kimkoa | 429 |
| 3. | Kitaifa | 8518 |
| 4. | Kimataifa | 631 |
| | **Jumla** | **10,120** |

**Umbo 2.2.2: Usajili wa Mashirika Kufikia Desemba, 2024**




## 2.3 Mahitaji ya Kisheria na Kikanuni Baada ya Usajili

Katika utekelezaji wa shughuli zake, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanapaswa kuzingatia mahitaji ya msingi ya kisheria na kikanuni kama ifuatavyo:

- Kuwasilisha taarifa za robo mwaka kwa mujibu Kanuni ya 20 ya Marekebisho ya Kanuni za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali za mwaka 2019 (Tangazo la Serikali Na. 685/2019).
- Kuwasilisha taarifa za mwaka za utekelezaji na za fedha zilizokaguliwa kwa mujibu wa Kifungu cha 29(1)(a) na (b) cha Sheria ya Mashirika Yasiyo ya kiiserikali, Sura ya 56 ya Sheria za Tanzania.
- Kufanya malipo ya ada ya usajili nay a mwaka kwa mujibu wa Kifungu cha 38(2)(b) cha Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sura ya 56 ya Sheria za Tanzania.
- Kuweka wazi taarifa za vyanzo vya mapato na uwasilishaji wa mikataba ya ufadhili kwa mujibu wa Kanuni ya 13(a), (b) na (c) ya Marekebisho ya Kanuni za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali za mwaka 2018 (Tangazo la Serikali, 608/2018).
- Kuhuisha taarifa za mabadiliko mbalimbali kwa mujibu wa Kifungu cha 33 cha Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sura ya 56.

- Kuandaa Mpango Mkakati wa Uendelevu wa Shirika, kutunza Rejesta ya Mali na kuweka sera za ndani za Shirika kwa mujibu wa Kanuni ya 14 ya Marekebisho ya Kanuni za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali za mwaka 2018 (Tangazo la Serikali, 608/2018).

## 2.4 **Uwasilishaji wa Taarifa na Ulipaji wa Ada**

Kwa mwaka 2024, jumla ya Mashirika Yasiyo a Kiserikali 1,360 yaliwasilisha taarifa za utekelezaji na taarifa za fedha zilizokaguliwa kati ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 9,279 yaliyopaswa kuwasilisha taarifa hizo. Idadi hiyo ni sawa na asilimia 14.6 ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yaliyopaswa kuwasilisha taarifa za mwaka 2024.


Vilevile, jumla ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 3,431 yamelipa ada za mwaka 2024 kati ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 9,279 yaliyotakiwa kulipa ada katika kipindi husika, ikiwa ni sawa na asilimia 36. Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, baadhi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yalifanya malipo ya ada ya mwaka, lakini hayakuwasilisha taarifa.

Kwa kiasi kikubwa, hali hiyo inapunguza utambuzi wa mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika maendeleo ya Taifa. Jedwali 2.4.1 na Umbo 2.4.1 yamefafanua zaidi kuhusu idadi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yaliyolipa ada na kuwasilisha taarifa katika ngazi mbalimbali za usajili kama inayoonekana hapo chini:

**Jedwali 2.4.1: Mashirika Yaliyolipa Ada na Kuwasilisha Taarifa**

| Na. | Ngazi ya Usajili | Mashirika Yaliyolipa Ada | Mashirika Yaliyowasilisha Taarifa |
|---|---|---|---|
| 1. | Kiwilaya | 150 | 45 |
| 2. | Kimkoa | 98 | 37 |
| 3. | Kitaifa | 2,780 | 1,030 |
| 4. | Kimataifa | 407 | 248 |
| | **Jumla** | **3,435** | **1,360** |

**Umbo 2.4.1: Mashirika Yaliyolipa Ada na Kuwasilisha Taarifa**





Aidha, kwa mwaka 2024, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 186 yaliwasilisha mikataba au hati za makubaliano ya ufadhili wa miradi kwa mujibu wa Kanuni ya 13(a) ya Marekebisho ya Kanuni za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali za mwaka 2018 (Tangazo la Serikali, 608/2018). Jumla ya mikataba 405 yenye kiasi cha shilingi 372,074,667,470 iliwasilishwa, kufanyiwa uchambuzi na kuidhinishiwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi na afua mbalimbali kama ilivyoainishwa kwenye jedwali 2.4.2 na Umbo 2.4.2

**Jedwali 2.4.2: Idadi ya Mikataba Iliyowasilishwa na Kuidhinishwa**

| Na. | Sekta/Afua | Idadi ya Mikataba | Kiasi Kilichoidhinishwa |
|---|---|---|---|
| 1 | Elimu | 63 | 46,847,466,521 |
| 2 | Afya | 47 | 44,886,209,005 |
| 3 | Maji | 16 | 22,551,270,569 |
| 4 | Nishati | 2 | 2,038,774,000 |
| 5 | Utawala Bora | 30 | 10,831,895,479 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 6 | Uwezeshaji wa Jamii | 96 | 60,028,175,565 |
| 7 | Jinsia | 15 | 13,423,962,500 |
| 8 | Ulinzi wa Jamii | 29 | 18,640,943,726 |
| 9 | Mazingira | 52 | 28,288,723,936 |
| 10 | Kilimo | 33 | 89,062,796,410 |
| 11 | Haki za Binadamu | 22 | 35,474,449,759 |
| **Jumla** | | **405** | **372,074,667,470** |

**Umbo 2.4.2: Asilimia ya Mikataba Iliyowasilishwa na Kuidhinishwa**



# SURA YA TATU

# UIMARISHAJI WA MAZINGIRA WEZESHI YA UTENDAJI KAZI WA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI

## 3.1 Utangulizi

Katika siku za hivi karibuni, Wizara kupitia Ofisi ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali imechukua hatua mbalimbali za kuimarisha mazingira wezeshi ya utendaji kazi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Hatua hizo zimesaidia kuimarisha misingi ya uwazi na uwajibikaji, kuongeza fursa za ufadhili na kuimaarisha uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, kuboresha uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, pamoja na kuongeza utambuzi wa mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika nyanja mbalimbali.

## 3.2 Mwongozo wa Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali

Katika jitihada za kuboresha uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali nchini, Wizara yenye dhamana ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, kwa kushirikiana na Wizara, Idara na Taasisi za Serikali, pamoja na Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO), imeboresha Mwongozo wa Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Tanzania Bara wa mwaka 2020 kupitia Toleo Jipya la mwezi Agosti, 2024.

Kupitia Mwongozo huo, Wizara, Idara na Taasisi za Kisekta zimepewa jukumu la kuwezesha Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutambua fursa zilizopo, mipango na vipaumbele vya Kitaifa, kutoa miongozo ya Kisera, na kusimamia utekelezaji wa miradi kwa kuzingatia viwango vya kitaalam vinavyohitajika ili kuhakikisha kuwa afua zinazotekelezwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali zinaendana na malengo ya Taifa.

Kwa upande mwingine, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanawajibika kuwasiliana na Wizara, Idara na Taasisi husika kabla ya kuanza kwa utekelezaji wa miradi na afua zake Hatua hiyo ni muhimu ili kubaini maeneo yenye uhitaji mkubwa na kupata mwongozo wa kisera na

kitaalam ili kuhakikisha kuwa miradi yao inakuwa na mchango chanya kwa jamii na inalingana na vipaumbele vya maendeleo ya Kitaifa.

### 3.3 Mkakati wa Uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali

Mkakati wa Kitaifa wa Uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 2022/23–2026/27 ulizinduliwa rasmi tarehe 04 Oktoba, 2022 na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa maelekezo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ***Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan***, aliyoyatoa tarehe 30 Septemba, 2021 wakati wa kilele cha Jukwaa la Mwaka la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kilichofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete Jijini Dodoma.

Mkakati huo unalenga kujenga uwezo thabiti kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili yaweze kuwa na uhimilivu wa muda mrefu na kujitegemea kiuchumi. Aidha, Mkakati unalenga kuimarisha mazingira wezeshi ya ndani yatakayowezesha Mashirika hayo kuendelea na shughuli zake kwa ufanisi, hata baada ya kumalizika kwa ufadhili wa nje. Vilevile, unalenga kupanua wigo wa mitindo ya ufadhili kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili yaweze kukidhi mahitaji yao ya kifedha, pamoja na kuimarisha uwezo wa utekelezaji wa dira, dhima na malengo ya Mashirika hayo kwa manufaa ya jamii na maendeleo ya Taifa.

### 3.4 Mfumo wa Kielektroniki wa Usajili na Uratibu wa Mashirika

Mfumo wa Kielektroniki wa Usajili na Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (*NIS*) ulianza kutumika rasmi mwezi Mei, 2020 kwa lengo la kuongeza ufanisi na kuimarisha uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kati ya Ofisi ya Msajili, Wizara za kisekta, Washirika wa Maendeleo, na Sekta Binafsi. Mfumo huo umeunganishwa na mifumo mingine ya Serikali kama vile Mfumo wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) na Mfumo wa Kielektroniki wa Malipo Serikalini (GePG). Kupitia mfumo huu, shughuli mbalimbali zinafanyika kwa njia ya kidijitali, zikiwemo usajili wa Mashirika, uwasilishaji na uhuishaji wa taarifa, pamoja na ulipaji wa ada.

Aidha, mwaka 2023, Wizara kwa kushirikiana na Wizara, Idara na Taasisi za Serikali, Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO), Sekta Binafsi na Washirika wa Maendeleo, iliboresha Mfumo wa NIS kwa kuongeza kipengele cha Ramani ya Kidijitali ya Utambuzi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (*NGOs Digital Mapping Tool*), ambayo ilizinduliwa rasmi na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, tarehe 05 Oktoba, 2023, wakati wa Jukwaa la Mwaka la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

Kupitia Ramani hiyo ya kidijitali, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanaweza kuonekana kirahisi katika maeneo yanayotekeleza miradi yao, pamoja na kutoa taarifa kuhusu aina ya miradi, rasilimali walizonazo, na walengwa wa miradi hiyo. Vilevile, ramani hii inaleta fursa kwa Mashirika kutangaza kazi zao, kuimarisha uwazi na uwajibikaji, pamoja na kuongeza uwezekano wa ubia na ufadhili kutoka kwa taasisi mbalimbali, kwa kutumia teknolojia rahisi na bunifu. Mfumo huu ni kichocheo muhimu cha uendelevu, ushirikiano na upatikanaji wa taarifa kwa wakati.

## 3.5 **Madawati ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali**

Kwa kuzingatia kuwa Sekta ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ni mtambuka na inagusa maeneo mbalimbali ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi, Wizara yenye dhamana ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali imeanzisha Madawati ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Wizara za Kisekta. Lengo la kuanzishwa kwa madawati haya ni kuboresha uratibu wa shughuli za Mashirika, kuongeza ufanisi katika utendaji kazi, na kuhakikisha utekelezaji wa miradi unazingatia vipaumbele vya Taifa.

Madawati hayo yalizinduliwa rasmi na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), tarehe 04 Oktoba, 2022, wakati wa kilele cha Jukwaa la Mwaka la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali lililofanyika Jijini Dodoma. Waratibu wa Madawati hayo katika Wizara za Kisekta, Wasajili Wasaidizi na Viongozi wa Mashirika, wamepewa uwezo wa kuingia na kutumia Mfumo wa NIS. Hii

inawawezesha kupata na kubadilishana taarifa kwa urahisi, kufanya ufuatiliaji wa shughuli, na kurahisisha mawasiliano baina ya wadau.

Hatua inayoendelea kwa sasa ni uanzishashwaji wa Madawati ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Taasisi nyingine za Serikali pamoja na Sekta Binafsi, ili kuongeza wigo wa uratibu na kuhakikisha ushirikiano jumuishi unaowezesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa ufanisi na uwazi zaidi.

### 3.6 Majukwaa ya Mwaka ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali

Jukwaa la Mwaka la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali lilizinduliwa rasmi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ***Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan***, tarehe 30 Septemba, 2021 jijini Dodoma. Lengo la Jukwaa hili ni kuendeleza ushirikiano wa karibu baina ya Serikali, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sekta Binafsi, na Washirika wa Maendeleo katika kuimarisha maendeleo ya Taifa.

Katika miaka iliyofuata, viongozi mbalimbali wa Kitaifa waliendelea kuwa wageni rasmi wa Jukwaa hili, jambo linalodhihirisha umuhimu wake Kitaifa. Mnamo tarehe 03 na 04 Oktoba, 2022, Waziri Mkuu Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) alikuwa Mgeni Rasmi wa Jukwaa hilo. Aidha, Jukwaa lililofanyika tarehe 03 hadi 05 Oktoba, 2023 lilihudhuriwa na Makamu wa Rais Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango kama Mgeni Rasmi, wakati Jukwaa la mwaka 2024, lililofanyika kuanzia tarehe 04 hadi 06 Septemba, likifunguliwa rasmi na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb).

Kwa kawaida, Jukwaa la Mwaka hutanguliwa na Majukwaa katika ngazi za Wilaya na Mikoa, ambapo hutoa fursa kwa wadau mbalimbali kujadiliana na kubadilishana uzoefu kuhusu fursa na changamoto zinazokumba utekelezaji wa shughuli za Mashirika. Vilevile, huambatana na mafunzo ya kujengeana uwezo, kutambua Mashirika yaliyofanya vizuri, pamoja na kuandaa maazimio ya kushughulikia changamoto zilizoibuliwa ili kuboresha utendaji wa Sekta ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali nchini.

## 3.7 Vikao Kazi vya Kisekta kati ya Wizara na Mashirika

Vikao Kazi vya Kisekta kati ya Wizara na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ni sehemu muhimu ya utekelezaji wa matakwa ya Mwongozo wa Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Tanzania Bara wa mwaka 2020 uliofanyiwa maboresho mwaka 2024.

Lengo la vikao kazi hivyo ni kuimarisha ushirikiano na mawasiliano baina ya Wizara yenye dhamana ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Wizara, Idara na Taasisi za Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, pamoja na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, ili kuhakikisha utekelezaji wa miradi ya Mashirika unaendana na vipaumbele vya Taifa. Katika utekelezaji wa Mwongozo huo, mwaka 2024 vilifanyika vikao vifuatavyo:

- Mwezi Julai 2024, kilifanyika kikao kazi cha Mashirika yanayotekeleza miradi na afua za maji mkoani Morogoro, ikiwa ni maandalizi ya mpango kazi wa uandaaji wa taarifa ya mchango wa wadau mbalimbali katika sekta ya maji;
- Mwezi Desemba, 2024, kilifanyika kikao kazi cha Mashirika yanayotekeleza miradi na afua za elimu mkoani Dar es Salaam, kwa lengo la kusaidia wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Vikao hivyo vimekuwa ni fursa muhimu ya kutathmini utekelezaji wa shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kisekta, kubadilishana uzoefu, kubaini changamoto na kuweka mikakati ya pamoja ya kuboresha utoaji wa huduma kwa jamii.

## 3.8 Ziara za Kujifunza na Kubadilishana Uzoefu wa Uratibu

Tarehe 16 Februari, 2021 wataalam kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Mamlaka ya Usimamizi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGORA) na Baraza la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (CONGOMA) nchini Malawi, walifanya ziara ya kujifunza na kubadilishana uzoefu wa uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali nchini Tanzania. Vilevile, tarehe 03 Oktoba,

2023 Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali nchini Uganda, alishiriki Jukwaa la Mwaka la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Jijini Dodoma.

Kama sehemu ya mwendelezo wa ziara hizo za kujifunza na kubadilishana uzoefu, tarehe 31 Julai hadi 03 Agosti, 2024 wataalam kutoka Ofisi ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Nchini Tanzania walifanya ziara ya kujifunza na kubadilishana uzoefu kuhusu uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Ofisi za Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Jiji la Kampala nchini Uganda.

Aidha, tarehe 04 hadi 06 Septemba, 2024 wawakilishi wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii Nchini Malawi, Mamlaka ya Usimamizi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGORA) na Taasisi ya Usajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Nchini Uganda walishiriki Jukwaa la Mwaka la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali lililofanyika Jijini Dodoma.

## SURA YA NNE

## VYANZO VYA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA ZA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI

### 4.1 Utangulizi

Kwa mujibu wa Kifungu cha 29 (1) (a) na (b) ya Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sura ya 56 ya Sheria za Tanzania, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yana wajibu wa kuwasilisha taarifa za mwaka za utekelezaji na taarifa za fedha zilizokaguliwa. Kupitia uchambuzi wa taarifa hizo, Wizara kupitia Ofisi ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali inaweza kubainisha kiwango cha fedha kilichopokelewa na kutumiwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika mwaka husika, pamoja na mikakati mbalimbali ya uendelevu wa Mashirika hayo.

### 4.2 Mapato ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali


Uchambuzi unaonesha kuwa katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Desemba 2024, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 1,360 yaliyowasilisha taarifa yake kwa ukamilifu yalipata fedha kiasi cha Shilingi 1,449,748,642,857 kutoka katika vyanzo mbalimbali vya fedha. Aidha, kiasi hicho cha mapato ya fedha za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Desemba, 2024 ni sawa na asilimia 09 ya Bajeti ya Serikali ya mwaka wa fedha 2024/2025. Mchanganuo wa vyanzo vya mapato ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa mwaka 2024 yameainishwa kwenye Jedwali 4.2 na Umbo 4.2 hapo chini.

**Jedwali 4.2: Vyanzo vya Mapato ya Mashirika**

| Na. | Aina ya Mapato | Kiasi | Asilimia |
|---|---|---|---|
| 1. | Bakaa | 28,573,425,405 | 1.97% |
| 2. | Msamaha wa Kodi | 72,960,289 | 0.01% |
| 3. | Ruzuku kutoka Serikalini | 1,775,402,079 | 0.12% |
| 4. | Michango ya Wanachama | 10,990,013,428 | 0.76% |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 5. | Mapato ya Vitega Uchumi | 12,384,448,084 | 0.85% |
| 6. | Malipo ya Huduma | 1,514,422,348 | 0.10% |
| 7. | Michango ya Jamii | 11,679,208,240 | 0.81% |
| 8. | Wafadhili wa Ndani | 13,921,245,183 | 0.96% |
| 9. | Michango kutoka Sekta Binafsi | 6,048,125,018 | 0.42% |
| 10. | Wafadhili wa Nje | 1,362,789,392,783 | 94.00% |
| **Jumla** | | **1,449,748,642,857** | **100%** |

**Umbo 4.2: Vyanzo vya Mapato ya Mashirika**




Taarifa hii ya mapato inaonesha kuwa, asilimia 94% ya mapato ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanategemea fedha kutoka kwa wafadhili wa nje. Aidha, michango ya wafadhili wa ndani katika utekelezaji wa miradi na afua mbalimbali za kusaidia jamii kwa mwaka 2024 imepungua. Hata hivyo, nguvu zaidi inatakiwa kuelekezwa kwenye eneo la mapato ya vitega uchumi, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ambao utayawezesha Yasiyo ya Kiserikali kuwa na vyanzo vya kudumu vya mapato.


### 4.3 Matumizi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali

Uchambuzi unaonesha kuwa katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Desemba 2024, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yalitumia kiasi cha Shilingi 1,289,344,177,596 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi pamoja na malipo ya posho na mishahara, pamoja na kodi mbalimbali za Serikali kama ilivyoainishwa katika Jedwali 4.3 na Umbo 4.3 hapo chini:

**Jedwali 4.3: Matumizi ya Fedha za Mashirika**

| Na | Aina ya Matumizi | Kiasi | Asilimia |
|---|---|---|---|
| 1. | Utekelezaji wa Miradi | 980,386,500,732 | 76.04% |
| 2. | Posho na Mishahara | 228,804,362,209 | 17.75% |
| 3. | Kodi ya Uendelezai wa Ujuzi (SDL) | 2,512,887,034 | 0.19% |
| 4. | Kodi ya Mishahara (PAYE) | 40,244,269,037 | 3.12% |
| 5. | Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) | 32,128,964,990 | 2.49% |
| 6. | Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) | 5,267,193,594 | 0.41% |
| **JUMLA** | | **1,289,344,177,596** | **100%** |

**Umbo 4.3 Matumizi ya Fedha za Mashirika**



Uchambuzi wa matumizi ya fedha zilizopokelewa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa mwaka 2024 unaonesha kuwa asilimia 76.04 ya fedha zilizopokelewa ilitumika katika utekelezaji wa miradi, asilimia 17.75 ulipaji wa posho na mishahara na asilimia 6.21 ilitumika katika ulipaji wa tozo na kodi mbalimbali za Serikali, ikiwemo Kodi ya Ujuzi (SDL), Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Kodi ya Mishahara (PAYE) na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF).

## SURA YA TANO

## MCHANGO WA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI KATIKA NYANJA MBALIMBALI ZA MAENDELEO

### 5.1 Utangulizi

Kama ilivyoelezwa kwenye Sura ya Kwanza ya taarifa hii, mwaka 2001, Serikali ilitunga Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili kuweka mazingira wezeshi kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kuleta mabadiliko mbalimbali ya kiuchumi na kijamii. Aidha, Sera hiyo imeweka misingi thabiti ya utambuzi wa mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika nyanja mbalimbali za maendeleo na Taifa kwa ujumla kupitia utekelezaji wa Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sura ya 56 na Kanuni zake.

Katika utekelezaji wa shughuli zake, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yana wajibu wa kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni, Malengo, Mipango na Mikakati mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa, ikiwemo Sera ya Maendeleo ya Jamii (1996), Sera ya Taifa ya Maji (2002), Sera ya Taifa ya Hifadhi ya Jamii (2003), Sera ya Afya (2007), Sera ya Taifa ya Kilimo (2013), Mpango wa Kitaifa wa Haki za Binadamu (2013), Sera ya Elimu na Mafunzo (2014), Sera ya Taifa ya Mazingira (2021), Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake (2023), Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (2020), Dira ya Maendeleo ya Taifa (2025), Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22-2025/26, pamoja na Malengo ya Maendeleo Endelevu (2030)

### 5.2 Utekelezaji wa Miradi na Afua Kisekta


Katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Desemba 2024, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 1,360 yalitumia kiasi cha Shilingi 1,289,344,177,596 katika utekelezaji wa miradi na afua mbalimbali, pamoja na masuala ya kiutawala. Kati ya fedha hizo, kiasi cha Shilingi 980,386,500,732 kilitumika kutekeleza miradi takribani 2,810 katika sekta ya elimu, uwezeshaji wa jamii, afya, mazingira, elimu, ulinzi wa jamii, kilimo,

utawala bora, maji, haki za binadamu, jinsia, nishati na miundombinu na viwanda kama inavyoonekana kwenye Jedwali 5.2 na Umbo 5.2.

**Jedwali 5.2: Idadi ya Miradi na Fedha Zilizotumika Kisekta**

| Na. | Sekta/Afua | Idadi ya Miradi | Kiasi Kilichotumika |
|---|---|---|---|
| 1. | Uwezeshaji wa Jamii | 731 | 370,820,898,559 |
| 2. | Afya | 469 | 291,303,490,749 |
| 3. | Mazingira | 221 | 80,863,674,279 |
| 4. | Elimu | 558 | 76,322,945,446 |
| 5. | Ulinzi wa Jamii | 304 | 57,337,725,511 |
| 6. | Kilimo | 117 | 49,846,109,010 |
| 7. | Utawala Bora | 99 | 21,633,125,580 |
| 8. | Maji | 69 | 12,073,361,551 |
| 9. | Haki za Binadamu | 131 | 10,504,562,411 |
| 10. | Jinsia | 99 | 8,937,949,113 |
| 11. | Nishati | 7 | 539,550,868 |
| 12. | Miundombinu | 3 | 199,907,655 |
| 13. | Viwanda | 2 | 3,200,000 |
| **Jumla** | | **2,810** | **980,386,500,732** |

**Umbo 5.2: Asilimia ya Fedha Zilizotumika katika Miradi Kisekta**



### 5.2.1 **Uwezeshaji wa Jamii**

Sambamba na malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa (2025), sehemu ya 2.5.3 ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26, pamoja na mambo mengine imejielekeza kuimarisha uwezeshaji jamii na mipango ya maendeleo ya sekta binafsi; kuhamasisha ushirikishwaji na uwezeshaji kiuchumi kwa watu wenye ulemavu na tabia ya kuweka akiba na kuwekeza katika shughuli za uzalishaji; pamoja na kuimarisha usimamizi wa mifuko ya uwezeshaji wa wananchi kiuchumi.

Kwa kuzingatia kuwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ni moja ya wadau muhimu katika kuiwezesha jamii na kuimarisha uwezo wao wa kujitegemea, katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Desemba 2024, sekta ya uwezeshaji wa jamii kiuchumi imeongoza kwa kutumia kiasi cha Shilingi 370,820,898,559 kutekeleza miradi 731 iliyolenga kutoa elimu ya ujasiriamali kwa vikundi vya vijana na wanawake kuhusu fursa mbalimbali za kiuchumi, ikiwemo mikopo ya Halmashauri (4/4/2).

Miradi na afua nyingine zililenga uwezeshaji katika afua za mazingira, elimu, kilimo, kuwajengea uwezo wanawake na vijana kwenye masuala ya ujasiliamali, na elimu ya uraia, kuwasaidia wanawake wajane, watoto wanaoishi katika mazingira magumu, watu wenye mahitaji maalum uzalishaji na uongezaji thamani kwenye bidhaa na mazao ya kilimo, pamoja na fursa za ajira hususani kwa vijana.

Washirika wa maendeleo walioongoza kufadhili miradi na afua za uwezeshaji wa jamii ni pamoja na Shirika la Maendeleo la Norway (NORAD), *Sevde Sevan Usak Vakfi, Convoy of Hope US, DOEN Foundation*, *Kijana Kwanza UK*, Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Umoja wa Ulaya (EU), *SwissContact, Girls Foundation US, GN Global Partnership Center, GN Global Impact Foundation*, Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Chakula Duniani (WFP), Shirika la Marekani la Misaada ya Kimataifa (USAID), *Friedrich-Ebert-Stiftung, Helvetas Swiss Intercooperation* na Taasisi ya *Mastercard Foundation*.

### 5.2.2 **Sekta ya Afya**

Kama ilivyoainishwa kwenye Sera ya Afya ya mwaka 2007, sekta ya afya ni muhimu kwa maendeleo ya watu. Sekta hii inajumuisha miundombinu, wataalamu, vifaa na vifaa tiba, vitendanishi, dawa, tiba, kinga na bima ya afya. Vilevile, sehemu ya 5.5.2 ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26, pamoja na mambo mengine unalenga kuimarisha mifumo ya usimamizi, upatikanaji na utoaji wa huduma za afya, ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya kutolea huduma za afya na uhamasishaji wa matumizi ya bima ya afya.

Katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Desemba, 2024 sekta ya afya ilitumia kiasi cha Shilingi 291,303,490,749 kutekeleza miradi na afua za kuzuia maambukizi ya VVU/UKIMWI (HIV/AIDS), kukabiliana na matumizi ya dawa za kulevya, afya ya jamii, lishe, matibabu ya macho, fistula, kansa, kifua kikuu, tohara, utoaji wa viungo bandia, afya ya uzazi, maendeleo ya awali ya mtoto, afya ya mama na mtoto, elimu ya afya ya uzazi kwa vijana balehe, huduma ya chanjo na vifaa tiba.

Washirika wa maendeleo walioongoza kwa ufadhili ni pamoja na Kituo cha Kudhibiti Magonjwa (CDC), Shirika la Misaada la Marekani (USAID), Mpango wa Dharura wa Rais wa Marekani wa Kukabiliana na UKIMWI (PEPFAR), Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza (FCDO), *JHPIEGO*, Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Korea (KOICA), *MSI Reproductive Choices Tanzania*, Shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia Wakimbizi (UNHCR), *BPRM, H&B Agerup, Bloomberg Philanthropies*, Ubalozi wa Ufaransa, *MdM, World Vision, National Community Lottery Fund*, *Washington State University* na *Pact Tanzania*.

### 5.2.3 **Uhifadhi wa Mazingira**

Kama ilivyoainishwa kwenye Sera ya Taifa ya Mazingira (2021), mazingira na maliasili asilia ni tunu ya Taifa na msingi wa maendeleo endelevu. Kwa msingi huo, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo wa ndani na nje ya nchi, imeendelea kuimarisha mifumo mbalimbali ya

utunzaji na uhifadhi wa mazingira, pamoja na matumizi endelevu ya rasilimali asilia kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

Vilevile, sehemu ya 5.3.5 ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22-2025/26 imejielekeza kuhamasisha matumizi ya nishati jadidifu; kupunguza uchafuzi wa mazingira pamoja na athari zake; kuimarisha uwezo wa Taifa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi; kupunguza uharibifu wa ardhi; kuboresha upandaji wa miti kibiashara; na kuendeleza mikakati ya kupambana na ujangili, biashara haramu na uvunaji haramu wa rasilimali za wanyamapori na misitu.

Kwa kuzingatia kuwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ni washiriki muhimu katika ulinzi, uhifadhi na utunzaji wa Mazingira, katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Desemba 2024, sekta ya uhifadhi wa mazingira ilitumia kiasi cha Shilingi 80,863,674,279 kutekeleza miradi iliyolenga kuwezesha upandaji miti na uhifadhi wa misitu, utunzaji wa vyanzo vya maji, upandaji wa miti mashuleni, miradi ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi, uboreshaji wa hifadhi za Taifa, kujengea uwezo jamii katika utunzaji wa mazingira, uhifadhi wa fukwe za bahari, mito na maziwa pamoja na uhifadhi wa ndege na wanyamapori.

Washirika wa maendeleo walioongoza kwa ufadhili ni pamoja na Shirika la Jane Goodhall Institute, Shirika la Marekani la Misaada ya Kimataifa (USAID), *KopeLion USA, The Nature Conservancy,* Shirika la *World-Wide Fund (WWF)*, Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Sweden (SIDA), *Vi Agroforestry*, Umoja wa Ulaya (EU), *Frankfurt Zoological Society*, pamoja na Shirika la Maendeleo la Norway (NORAD).

### 5.2.4 **Sekta ya Elimu**

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yametekeleza miradi ya elimu hususani ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya elimu, ugawaji wa samani, vitabu na mahitaji mengine ya elimu. Kwa mwaka 2024, sekta ya elimu ilitumia kiasi cha Shilingi 76,322,945,446 zilizotekeleza miradi 503, ikiwemo utoaji wa ufadhili kwa watoto, kampeni ya kuzuia ukatili dhidi ya watoto,

programu ya kuwezesha watoto wa kike kubaki shuleni, ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya shule, kuwajengea uwezo walimu na utoaji wa vifaa kwa ajili ya elimu kama vile vitabu, kompyuta na sare.

Washirika wa maendeleo walioongoza kwa ufadhili ni pamoja na *Conrad N. Hilton Foundation*, *Room to Read*, *Young Life USA, BMZ, World Learning Ogranization, Malala Fund, USAID, Plan International, Opportunity Education Foundation, CAMFED, Village Schools International, KOICA, GN Global Partership Center* na *USDA*.



*Pichani ni Baadhi ya Majengo ya Shule ya Msingi Inayomilikiwa na Shirika la SHADE Mkoani Shinyanga.*

### 5.2.5 **Ulinzi wa Jamii**

Sehemu ya 5.5.6 ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22-2025/26 imejielekeza kuimarisha huduma za malezi mbadala ikiwemo malezi ya kambo na kuasili watoto, kuzuia na kutokomeza ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto; huduma za malezi, makuzi, maendeleo ya awali ya mtoto; na huduma za afya, unasihi na msaada wa kisaikolojia kwa makundi yenye uhitaji.

Kwa msingi huo, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yamechangia uanzishaji na uhamasishaji wa jamii katika kulinda maslahi na ustawi wa watoto, wazee, wajane, wanawake, vijana, watu wenye ulemavu na watoto

yatima hususani kupitia utekelezaji wa miradi ya uendeshaji wa makao ya watoto, huduma malezi ya awali kwa watoto, nyumba salama na vituo vya kulelea watoto wadogo mchana.

Katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Desemba 2024, sekta ya ulinzi wa jamii ilitumia kiasi cha Shilingi 57,337,725,511 kutekeleza miradi na afua za kusaidia watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi na kuwaunganisha na familia zao, elimu kwa watoto wanaoishi katika mazingira magumu, kuweka mazingira salama kwa watu wenye mahitaji maalum wanaoishi katika kambi za wakimbizi, pamoja na kutoa huduma ya maji, afya na lishe kwa familia zinazoishi katika mazingira hatarishi.

Washirika wa maendeleo walioongoza kwa ufadhili ni pamoja na *SOS Denmark, Rahma International Society,* Kampuni ya *Deloitte Consulting Ltd, FHI360, UNHCR, Integrated Security Fund (ISF), BMZ kupitia GFFO, UKAID, Liverpool Football Club Foundation, NORAD* na *GAC*.



*Pichani ni Jengo la Ofisi na Sehemu ya Malazi Katika Shule Inayomilikiwa na Shirika la Siouxland Tanzania Education Medical Ministries (STEMM) Mkoani Arusha.*

### 5.2.6 **Sekta ya Kilimo**

Kama ilivyoainishwa kwenye Sera ya Taifa ya Kilimo (2013), uchumi wa Tanzania umeendelea kutegemea zaidi kilimo, ijapokuwa mchango wake katika Pato la Taifa unaendelea kushuka. Sekta ya Kilimo imeendelea kuwa kitovu cha ukuzaji wa viwanda na maisha ya watu nchini, ambapo inakadiriwa kuwa kinaajiri takribani asilimia 66.3 ya nguvukazi, ambapo wanawake ni asilimia 52 na wanaume asilimia 48.

Aidha, sehemu ya 5.3.1 ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22-2025/26, imejielekeza kufungamanisha sekta ya kilimo na sekta nyingine za kiuchumi, kujenga mazingira mazuri kwa sekta binafsi kuendesha shughuli za uzalishaji na kuendelea kuimarisha programu za mafunzo. Hatua hizi, zinalenga kuongeza thamani na tija ya uzalishaji wa mazao ya kilimo, kuzalisha ajira, kutanua wigo mseto wa bidhaa na kuimarisha mnyororo wa thamani katika sekta ya kilimo.

Katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Desemba 2024, sekta ya kilimo ilitumia kiasi cha Shilingi 49,846,109,010 kutekeleza miradi ya kuwajengea uwezo vijana katika masuala ya kilimo, ufugaji wa kuku, utafiti, usambazaji wa pembejeo za kilimo, kuongeza thamani kwenye mazao, kuwajengea uwezo wakulima na Maafisa Ugani kuhusu uzalishaji wa mbegu bora, elimu kwa wanawake kuhusu matumizi ya mbinu za asili katika kilimo na upatikanaji wa masoko ya bidhaa za kilimo.

Washirika wa maendeleo walioongoza kwa ufadhili katika sekta ya kilimo ni pamoja na Taasisi ya *KopeLion USA, The Nature Conservancy, Geneva Federation for Cooperation (FGC),* Shirika la *World Wide Fund (WWF),* Shirika la Marekani la Misaada ya Kimataifa (USAID), Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Sweden (SIDA), Umoja wa Ulaya (EU), Shirika la *Frankfurt Zoological Society, Rockefeller Philanthropy* na Shirika la Maendeleo la Norway (NORAD).



*Pichani ni Shamba la Nyanya Linalomilikiwa na Shirika la Siouxland Tanzania Education Medical Ministries (STEMM) Mkoani Arusha.*

### 5.2.7 **Utawala Bora**

Mifumo ya utoaji na upatikanaji wa haki ni muhimu katika kuimarisha usawa na ustawi wa jamii. Utoaji na upatikanaji wa haki unawezekana ikiwa kuna mifumo imara ya kitaasisi. Mifumo hiyo inajumuisha watumishi wenye weledi, vitendea kazi, miundombinu wezeshi na miongozo rafiki katika utoaji haki. Kwa msingi huo, mifumo ya utoaji na upatikanaji wa haki ni moja ya nguzo muhimu za utawala bora.

Vilevile, sehemu ya 5.5.8 ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22-2025/26 imejielekeza kuboresha mifumo na miundombinu ya utoaji wa haki, kuhamasisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji na upatikanaji wa haki, pamoja na kuimarisha taratibu na miongozo ya utoaji wa msaada wa kisheria nchini. Aidha, baadhi ya malengo ya kimkakati ya Mpango Mkakati wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora wa Mwaka 2023-2026 ni pamoja na kuimarisha utekelezaji wa mikakati ya kitaifa ya kuzuia rushwa na kuimarisha uzingatiaji wa misingi ya utawala bora.

Katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Desemba 2024, sekta ya utawala bora ilitumia kiasi cha Shilingi 21,633,125,580 kutekeleza miradi kukuza utawala bora, kuwajengea uwezo vijana na wanawake kuhusu masuala ya uongozi, mafunzo kuhusu elimu ya uraia, kushawishi mabadiliko ya sera na sheria, haki za kiuchumi, haki za binadamu, uadilifu, uwazi na uwajibikaji na usaidizi wa masuala ya kisheria.

Washirika wa maendeleo walioongoza kwa ufadhili katika sekta ya utawala bora ni pamoja na *UNA Sweden*, *African Women Development Fund, Ford foundation, Hewlett foundation*, Ubalozi wa *Switzerland, SIDA, Hempel Foundation, EU, Global Health Advocacy Incubator (GHAI), Wellspring Philanthropic Fund, KAS* na *USAID*.

### 5.2.8 **Sekta ya Maji**

Kama ilivyoainishwa kwenye Sera ya Taifa ya Maji (2002), sekta ya maji inahusisha upatikanaji na usambazaji wa maji pamoja na utunzaji wa vyanzo vya maji. Vilevile, mpango wa maendeleo na usimamizi wa usambazaji wa maji vijijini na mijini unahitaji mahusiano ya kitaasisi miongoni mwa wadau muhimu ambao ni Serikali, Sekta Binafsi, Washirika wa Maendeleo, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na jamii kwa ujumla.

Vilevile, sehemu ya 5.5.3 ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22-2025/26 imetoa kipaumbele katika upatikanaji na usambazaji wa maji safi na salama vijijini na mijini, utunzaji wa vyanzo vya maji; uimarishaji wa miundombinu jumuishi ya upatikanaji na usambazaji wa maji safi na salama mijini na vijijini, pamoja na uimarishaji wa programu za uhifadhi wa vyanzo vya maji.

Katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Desemba 2024, sekta ya maji ilitumia kiasi cha Shilingi 12,073,361,551 kutekeleza miradi na afua mbalimbali, ikiwemo elimu ya afya na usafi wa mazingira mashuleni na kwenye jamii, uchimbaji wa visima vya maji vijijini na mijini, ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya maji, mafunzo kwa kamati za maji vijijini, uhifadhi wa vyanzo vya maji na uboreshaji wa huduma za maji.

Washirika wa maendeleo walioongoza kwa ufadhili katika sekta ya maji ni pamoja na Shirika la *Charity Water*, *Water Engineers for the Americans and Africa (WEFTA)*, Mfuko wa Kuhudumia Watoto wa Umoja wa Mataifa (UNICEF), Shirika la *Worldserve International*, Shirika la *Life Water International*, Umoja wa Ulaya (EU), Shirika la *Catholic Relief Services*, pamoja na Taasisi ya *Go Drill Inc*.

5.2.9 **Haki za Binadamu**

Kama ilivyoainishwa kwenye Mpango wa Kitaifa wa Haki za Binadamu (2013), sehemu ya 5.5.8 ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22-2025/26, pamoja na mambo mengine imejielekeza kuimarisha upatikanaji wa haki na ulinzi wa haki za binadamu nchini, pamoja na kuimarisha miongozo na taratibu za utoaji wa huduma ya misaada ya kisheria kwa wananchi.

Aidha, malengo ya kimkakati ya Mpango Mkakati wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora wa Mwaka 2023-2026 yamejikita kuimarisha afua za kukabiliana na VVU/UKIMWI na magonjwa yasiyoambukiza, kuimarisha utekelezaji wa mikakati ya kitaifa ya kuzuia rushwa, pamoja na kuimarisha ulinzi wa haki za binadamu.

Katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Desemba 2024, sekta ya haki za binadamu ilitumia kiasi cha Shilingi 10,504,562,411 kutekeleza miradi ya utoaji wa msaada wa kisheria, kampeni za kupinga ukatili wa kijinsia, kuwajengea uwezo na kutoa mafunzo ya kiuchumi na kisheria, kuhamasisha kulinda amani, kuelimisha kuhusu haki za kijamii na kiuchumi kwa wanawake na wasiojiweza, kuwajengea uwezo vijana na taasisi zinazotoa huduma ya msaada wa kisheria kwa jamii, pamoja na kutoa elimu ya utetezi na ushawishi kuhusu masuala ya haki za binadamu.

Washirika wa maendeleo walioongoza kwa ufadhili ni pamoja na Umoja wa Ulaya (EU), *WeWorld Online Foundation, Segal Family Foundation, TIDES Foundation, Better Way Foundation*, Shirika la *Protection International Africa (PIA)*, Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Sweden

(SIDA), *Ford Foundation, Wellspring Foundation*, Shirika la ***Well Spring Foundation***, pamoja na *Rights and Resources Group (RRG)*.

5.2.10 **Masuala ya Kijinsia**

Ushiriki wa wanawake katika nyanja mbalimbali ni muhimu ili kuleta usawa na kuondoa ukatili wa kijinsia. Ni kwa msingi huo, sehemu ya 2.5.3 ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22-2025/26 imejielekeza katika miradi na afua zenye lengo la kuleta usawa wa kijinsia kwa wanawake na wasichana, kuongeza fursa za elimu na mafunzo kwa wasichana, hatua za haraka dhidi ya ubaguzi katika masuala ya umiliki wa ardhi na urithi, unyanyasaji dhidi ya wanawake, pamoja na kuongeza elimu dhidi ya mila na tamaduni zinazomkandamiza mwanamke.

Vilevile, kwa mujibu wa sehemu ya 5.2.26 ya Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake (2023), Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yana wajibu wa kuingiza masuala ya kijinsia katika mipango yao, kuhamasisha ushiriki sawa wa wanawake na wanaume katika ngazi mbalimbali za maamuzi, pamoja na kuhamasisha utengaji wa bajeti kwa ajili ya mahitaji ya makundi maalum katika jamii hususan watu wenye ulemavu, watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi na watu wanaoishi na VVU/UKIMWI.

Katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Desemba 2024, sekta ya jinsia ilitumia kiasi cha Shilingi 8,937,949,113 kutekeleza miradi ya kuhamasisha masuala ya usawa wa kijinsia, kuwawezesha wanawake kijamii na kiuchumi, kuwajengea uwezo wasichana na wanawake kuhusu haki zao za msingi, elimu na kampeni za kupinga ukatili wa kijinsia na kwa watoto, masuala ya uongozi na utawala bora, nyumba salama, fursa za uongozi kwa wanawake, kuwaelimisha na kuwezesha watoto wa kike katika masuala ya hedhi salama na kubaki shuleni.

Washirika wa maendeleo walioongoza katika ufadhili wa miradi ni pamoja na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Sweden (SIDA), Mfuko wa Umoja wa Mataifa wa Idadi ya Watu (UNFPA), Ubalozi wa *Ireland*, *Project Management Institute Education Fund,* Taasisi ya ***Global Affairs Canada***

*(GAC),* Shirika la Marekani la Misaada ya Kimataifa (USAID), pamoja na *Women Fund Tanzania Trust*.



*Pichani ni Kiwanda cha Kutengeneza Taulo za Kike za Kufua cha Tabasamu la Malkia, Kinachomilikiwa na Shirika la Humuliza Mkoani Kagera.*

## 5.3 Wanufaika wa Miradi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali


Katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Desemba 2024, miradi na afua ziilizotekelezwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali imenufaisha makundi mbalimbali katika jamii. Uchambuzi unaonesha kuwa makundi yaliyoongoza kwa kufikiwa zaidi na miradi au afua zilizotekelezwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ni Vijana ambao walifikiwa kwa takribani asilimia 42 na Wanawake ambao walifikiwa kwa takribani asilimia 23.

Aidha, uchambuzi unaonesha kuwa kundi la wagane ndilo lililofikiwa kwa uchache zaidi na miradi iliyotekelezwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika kipindi husika. Vievile, jumla ya taasisi 3,141,796 zikiwemo Taasisi za Serikali na Sekta Binafsi zilifikiwa katika kipindi husika kama inayooneshwa kwenye Jedwali 5.3 na Umbo 5.3 hapo chini:

**Jedwali 5.3: Idadi ya Waliofikiwa na Miradi Mbalimbali**

| Na. | Aina ya Wanufaika | Jumla ya Wanufaika | Asilimia |
|---|---|---|---|
| 1. | Wanawake | 129,040,566 | 24.22% |
| 2. | Watoto | 55,079,807 | 10.34% |
| 3. | Wanaume | 46,970,640 | 8.81% |
| 4. | Wazee | 62,046,346 | 11.64% |
| 5. | Wajane | 15,816 | 0.00% |
| 6. | Vijana | 233,220,607 | 43.76% |
| 7. | Walemavu | 3,316,724 | 0.62% |
| 8. | Taasisi | 3,141,796 | 0.58% |
| 9. | Wagane | 149 | 0.00% |
| **Jumla** | | **532,832,451** | **100.00%** |

**Umbo 5.3: Asilimia ya Waliofikiwa na Miradi Mbalimbali**




## 5.4 Ajira Zilizozalishwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali

Uchambuzi unaonesha kuwa katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Desemba 2024, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 910 yalizalisha jumla ya ajira 18,526 ambapo kati ya hizo 12,403 (Watanzania 12,272 na Wageni 131) zilikuwa ajira rasmi na 6,126 (Watanzania 5,761 na wageni 365) zilizkuwa ajira za kujitolewa. Kati ya ajira hizo jumla ya ajira 10,504 zilikuwa za wanawake na 8025 zilikuwa za wanaume. Aidha, jumla ya Shilingi 245,004,730,237 zilitumika kulipa mishahara na posho za waajiriwa. Jedwali 5.4.1, Umbo 5.4.1 na Umbo 5.4.2 yameainisha idadi na mgawanyo wa waajiriwa katika makundi mbalimbali.


**Jedwali 5.4.1 Mgawanyo wa Idadi ya Waajiriwa**

| Na. | Kundi | Watanzania Walioajiriwa | Wageni Walioajiriwa | Watanzania Wanaojitolea | Wageni Wanaojitolea | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Vijana | 6,492 | 34 | 3,788 | 272 | 10,586 |
| 2. | Watu Wazima | 5,699 | 94 | 1,915 | 82 | 7,790 |
| 3. | Wazee | 81 | 3 | 58 | 11 | 153 |
| **Jumla** | | **12,272** | **131** | **5,761** | **365** | **18,529** |

**Umbo 5.4.1: Mgawanyo wa Idadi ya Waajiriwa**



**Umbo 5.4.2: Mgawanyo wa Ajira kwa Jinsia**




Uchambuzi unaonesha kuwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yamechangia kuajiri watu wapatao 18,529 kwa ujumla, Aidha Mashirika yaliyoongoza kwa kutoa ajira ni pamoja na Shirika la *Builders of Future Africa (BFA)* (963), Shirika la *Dr. Nicholaus Memorial Nature Conservation* (835), *Affirmative Action on Gender Equality Network (AGEN)* (806), Shirika la *Brac Maendeleo Tanzania* (539), Shirika la *World Vision Tanzania* (523), *The Foundation for Human Health and Social Development* (385).

## 5.5 Makato ya Kisheria ya Posho na Mishahara ya Waajiriwa

Katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Desemba 2023, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 199 yalichangia kiasi cha Shilingi 40,244,269,037 kupitia Kodi ya Mishahara (PAYE), Mashirika 263 yalichangia kiasi cha Shilingi 32,128,964,990 kupitia Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Mashirika 113 yalichangia kiasi cha Shilingi 2,512,887,034 kupitia Kodi ya Ujuzi (SDL) na Mashirika 239 yalichangia kiasi cha shilingi 5,267,193,594 kupitia Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF).

Aidha, uchambuzi unaonesha kuwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yaliyofanya vizuri ni pamoja na *MSPH Tanzania LLC, Tanzania Health Promotion Support (THPS), Amref Health Africa – Tanzania, World Vision Tanzania, JHPIEGO Corporation, BRAC Maendeleo Tanzania, Ubongo Learning, Right to Play, The Jane Goodall Institute* na *Pathfinder International.*

# SURA YA SITA

# UTEKELEZAJI WA MKAKATI WA KITAIFA WA UENDELEVU WA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI

## 6.1 Utangulizi

Mwaka 2022, Serikali ilizindua *Mkakati wa Kitaifa wa Uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (2022/23–2026/27)*. Uzinduzi huo ulifanywa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa agizo la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ***Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan***, alilolitoa tarehe 30 Septemba, 2021 wakati wa Jukwaa la Mwaka la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

## 6.2 Malengo

Kupitia mkakati huo, Serikali imelenga kujenga ikolojia endelevu ya kuimarisha uwezo wa kitaasisi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, kuongeza msingi wa kifedha na kuendeleza ushirikiano wa kimkakati kwa maendeleo ya muda mrefu. Mkakati huo unatumika kama dira ya kujenga uwezo thabiti wa Mashirika, utengamano wa kifedha, uhimilivu na ukuaji wa kifedha ili kufikia uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Malengo mahsusi ya Mkakati huo ni pamoja na:

- Kujenga uwezo thabiti wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuwa na uhimilivu na kujitegemea kiuchumi ifikapo mwaka 2026/27.
- Kuimarisha mazingira wezeshi ya ndani yanayosaidia uendelevu wa muda mrefu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanayofanya kazi Tanzania bara ifikapo mwaka 2026/27.
- Kupanua kwa wigo wa mitindo ya ufadhili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili kukidhi mahitaji yake ya ufadhili.
- Kuimarisha uwezo wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutekeleza dira, dhima na malengo yake ifikapo mwaka 2026/27.

## 6.3 Utekelezaji na Fursa Zilizopo

Utekelezaji wa Mkakati huu unahusisha juhudi za pamoja kutoka kwa Serikali na taasisi zake katika ufuatiliaji, kuweka mazingira wezeshi, na utatuzi wa migogoro. Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yana wajibu wa kuandaa mipango ya utekelezaji, Sekta binafsi inatekeleza kupitia dhana ya Uwajibikaji kwa Jamii (CSR) na Jamii na wadau wa maendeleo wanashiriki kupitia usaidizi wa kimkakati na kiufadhili.

Baadhi ya vipengele muhimu vinavyochangia mafanikio katika utekelezaji wa Mkakati huo ni pamoja na kuanzishwa kwa miradi ya uzalishaji mali, ushirikiano wa kimkakati, ubunifu wa programu, matumizi ya teknolojia na uwekezaji wa ndani wa kimkakati kupitia umiliki na uendelezaji wa ardhi, majengo na utoaji wa huduma.

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali nchini Tanzania yana fursa za kutosha katika utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, ikiwemo Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2001, Mwongozo wa Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Tanzania Bara Toleo la mwaka 2024 na Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Sura ya 56 ya Sheria za Tanzania.

## 6.4 Tathmini ya Utekelezaji wa Mkakati

Kwa kutumia taarifa za utekelezaji wa miradi kwa robo mwaka, mwaka, mikataba ya fedha, pamoja na mifumo ya ufuatiliaji na tathmini, imebainika kuwa Mashirika kadhaa yamefanikiwa kwa kiwango cha juu katika utekelezaji wa mkakati wa uendelevu. Tathmini hii inaangazia miradi mbalimbali iliyotekelezwa na Mashirika katika sekta za elimu, afya, kilimo, nishati, teknolojia, na huduma za jamii.

## 6.5 Mafanikio ya Utekelezaji wa Mkakati

Tangu mkakati huu uzinduliwe, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yameboresha uwezo wa kiutendaji kwa kupunguza utegemezi wa wafadhili, kuboreshwa kwa mifumo ya usimamizi, kuanzishwa kwa

ushirikiano mpya (taasisi za kifedha, sekta binafsi) na uanzishaji wa miradi ya uzalishaji mali inayowezesha kujitegemea.

### 6.5.1 **Umiliki wa Majengo na Miundombinu**

Miradi hii inahusisha ofisi, shule, hospitali na majengo ya biashara, kama inavyoonekana kwenye Jedwali 6.5.1 hapo chini.

**Jedwali 6.5.1 Umiliki wa Majengo na Miundombinu**

| Na. | Shirika | Mkoa | Mradi |
|---|---|---|---|
| 1. | Community Economic Empowerment and Legal Support (CEELS) | Rukwa, Katavi | Jengo la Ofisi katika Wilaya ya Nkasi na Mpanda. |
| 2. | Tanzania Women Architects and Engineers (TAWAH) | Kilimanjaro | Nyumba ya Makazi, Kituo cha ubunifu na mafunzo ya ujenzi kwa wanawake. |
| 3. | Comprehensive Community Based Rehabilitation Tanzania (CCBRT) | Dar es Salaam | Hospitali inayotoa huduma za macho, mifupa na viungo na afya ya uzazi. |
| 4. | Rural Development Organization (RDO) | Iringa | Vyuo vya ufundi (VTCs) na Nyumba ya kulala wageni (RDO Jamii Lodge) |
| 5. | Tanzania Gender Networking Programme (TGNP) | Dar es Salaam | Majengo na ukumbi wa kupangisha |
| 6. | PELUM Tanzania | Morogoro | Jengo la ofisi |
| 7. | Sawa Wanawake Tanzania | Morogoro | Jengo kwa ajili ya Ofisi na Shule |
| 8. | Eternal Families | Tabora | Nyumba za Makazi na Shule |
| 9. | Ilula Orphans Program | Iringa | Shule, Chuo cha ufundi, Maktaba, Nyumba za malazi, Mgahawa, Ukumbi wa Sherehe na Duka. |
| 10. | Intergrated Rural Development Organization (IRDO) | Songwe | Hosteli |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 11. | Africraft NGO | Dar es salaam | Nyumba za kulala wageni |
| 12. | Chama Cha Uzazi Na Malezi Bora Tanzania (UMATI) | Dar es salaam | Majengo ya kupangisha |
| 13. | Amani Girls Organization | Mwanza | Shule |
| 14. | Pastoralists Livelihood Support and Empowernment Programme (PALISEP) | Arusha | Kituo cha shughuli Stadi za Maisha |
| 15. | Hope For Girls and Women in Tanzania (HGWT) | Mara | Nyumba salama |
| 16. | Project Watu Kamili Inc. | Kilimanjaro | Kituo cha shughuli Stadi za Maisha |
| 17. | German Foundation for World Population (DSW) Tanzania | Arusha | Kituo cha uwezeshaji vijana |
| 18. | The School of St. Jude | Arusha | Shule |
| 19. | African Relief Organization | Dar es salaam | Shule |
| 20. | Life Education Tanzania (LET) | Pwani | Kituo cha kulelea watoto mchana (Day care) |
| 21. | SOS Children's Villages Tanzania | Dar es salaam | Nyumba |
| 22. | Vijaliwa vingi | Pwani | Shule |
| 23. | The Bishop Samson Mushemba Foundation | Kagera | Shule |
| 24. | Shade | Shinyanga | Shule |
| 25. | Health Promotion Tanzania | Dar es salaam | Mradi wa Mwani na Ukumbi wa Mikutano |
| 26. | Mama's Hope Organization for Legal Assistance (MHOLA) | Kagera | Hosteli ya kupangisha |
| 27. | Kamer Foundation | Pwani | Shule |
| 28. | Tumaini Jipya la Wanawake Kilwa | Lindi | Ukumbi wa Mikutano na fremu za biashara |
| 29. | Amani Centre for Street Children | Kilimanjaro | Kituo cha kulea watoto |

### 6.5.2 **Uanzishaji wa Taasisi za Kifedha**

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kama *Brac Maendeleo Tanzania, World Vision Tanzania, Foundation for Civil Society (FCS)* na *Mara Empowerment Assistance* yameanzisha taasisi za kifedha ili kupanua wigo wa mapato, kama inayoonekana katika Jedwali 6.5.2 hapo chini.

**Jedwali 6.5.2: Uanzishaji wa Taasisi za Kifedha**

| Na. | SHIRIKA | Mkoa | Mradi |
|---|---|---|---|
| 1. | Foundation for Civil Society (FCS) | Dar es salaam | FCS Trust |
| 2. | World Vision Tanzania | Arusha | VisionFund Tanzania Microfinance Bank |
| 3. | Brac Maendeleo Tanzania | Dar es salaam | Brac Tanzania Finance Limited |
| 4. | Mara Empowerment Assistance | Mara | Mara Women Empowerment Financial Service |

### 6.5.3 **Uwekezaji katika Kilimo na Ufugaji**

Mashirika yameweza kuwekeza katika miradi ya kilimo, na ufugaji kama njia muhimu ya kujiongezea kipato ambapo yameweza kufanya uzalishaji wa mazao ya biashara na chakula, kama inavyoonekana kwenye Jedwali 6.5.3 hapo chini.

**Jedwali 6.5.3: Uwekezaji katika Ardhi na Kilimo**

| Na. | Shirika | Mkoa | Mradi |
|---|---|---|---|
| 1. | Sioxland Tanzania Education Medical | Arusha | Kilimo cha mbogamboga |
| 2. | Southern Highlands Participatory Organization (SHIPO) | Njombe | Kilimo cha mbogamboga |
| 3. | Foundation of New Life for Street Children and Orphans - FONELISCO | Mwanza | Ardhi Hekari 70 na Ufugaji wa Ng'ombe |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 4. | Humuliza Organization - Psychosocial Support for Orphans and Vulnerable Children | Kagera | Ardhi hekari 24 |
| 5. | The Bishop Samson Mushemba Foundation | Kagera | Kilimo cha Vanilla |
| 6. | Ilula Orphans Program | Iringa | Shamba la Maparachichi |
| 7. | Lebao's Kids Foundation (BKF) | Iringa | Shamba la Maparachichi, Mbogamboga na Ufugaji wa Kuku |
| 8. | Rikolto Tanzania | Arusha | Kilimo cha Maparachichi na Kivingulio |

6.5.4 **Miradi Mingine ya Kiubunifu na Kijamii**

Mashirika pia yameanzisha miradi ya ubunifu kama uzalishaji wa nishati, usindikaji wa mazao, vyombo vya habari, na elimu ya awali, kama inayoonekana kwenye Jedwali 6.5.4 hapo chini.

**Jedwali 6.5.4 Miradi Mingine ya Kiubunifu na Kijamii**

| Na. | Shirika | Mkoa | Mradi |
|---|---|---|---|
| 1. | CEFA - International Committee for Agriculture Training and Cooperation | Njombe | Ufuaji wa Nishati ya Umeme |
| 2. | Africraft NGO | Dar es salaam | Kampuni ya uzalishaji bidhaa kupitia taka (Made by Africraft) |
| 3. | Mviwata Ngazi ya Kati Morogoro | Morogoro | Redio |
| 4. | Support Makete to Self-Support (SUMASESU) | Njombe | Redio |
| 5. | Mikono Yetu Organization | Mwanza | Kiwanda cha kusindika maziwa, kutengeneza mikate na siagi ya karanga |
| 6. | Tanzania Early Childhood | Mwanza | Mashine ya Kukoboa na |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | Education and Care (TECEC) | | Kusaga mahindi. |
| 7. | Haki Elimu | Dar es salaam | Machapisho mbalimbali na Ushauri elekezi |
| 8. | Himiza Social Justice | Geita | Kampuni ya Mawakili ya Rafiki Attorneys |
| 9. | New Light Children Center Organization (NELICO) | Geita | Mfuko wa Maendeleo ya Shirika (Organization Development Fund) |
| 10. | Humuliza Organization - Psychosocial Support for Orphans and Vulnerable Children | Kagera | Kiwanda cha Tabasamu la Malkia ambacho kinatengeza taulo za kike za kufua<br>Kituo cha Radio Jamii |
| 11. | Mama's Hope Organization for Legal Assistance (MHOLA) | Kagera | Ukodishaji wa gari aina ya Coaster |

### 6.6 Changamoto za Utekelezaji wa Mkakati

Katika utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kumekuwa na changamoto ambazo zimekuwa zikijitokeza kama ifuatavyo:

- Baadhi ya Mashirika hayana mifumo imara ya ufuatiliaji na tathmini ya miradi yao, jambo ambalo linaathiri uendelevu wa matokeo na utekelezaji wa Mkakati kwa kiasi kikubwa.
- Ushirikiano hafifu kati ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na sekta binafsi unaopelekea Mashirika kukosa fursa mbalimbali zinazotolewa na Sekta binafsi kwa Mashirika kupitia Sera ya uwajibikaji kwa jamii (CSR Policy).
- Baadhi ya Mashirika hayana mpango kazi unaojumuisha utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Uendelevu kwa kuwa baadhi ya miradi inayotekelezwa haina mikakati ya muda mrefu ya kuendeleza mafanikio ya miradi baada ya ufadhili kukoma.
- Baadhi wa wafadhili kutokuweka kipaumbele katika utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali

na hivyo kusababisha Mashirika kukosa rasilimali fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mkakati huo.

## 6.7 **Mapendekezo**

Katika kukabiliana na changamoto zilizobainishwa hapo juu na kuhakikisha uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, inashauriwa kama ifuatavyo:

- Kuendelea kutoa elimu ya Mkakati kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kupitia majukwaa mbalimbali kama vile vikao kazi, makongamano, mitandao ya kijamii na vyombo vya habari.
- Kuimarisha ushirikiano kati ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Sekta Binafsi katika utekelezaji wa Sera ya Uwajibikaji kwa Jamii (Corporate Social Responsibility - CSR Policy).
- Kuhamasisha wafadhili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutenga kiasi cha fedha kwa ajili ya kuyawezesha Mashirika kutekeleza miradi yenye uendelevu.
- Kuendelea kusisitiza Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji na tathmini ya miradi yao hasa yenye matokeo ya muda mrefu.

# SURA YA SABA

# MWENENDO WA UFADHILI KWA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI KATIKA KIPINDI CHA MIAKA MITANO ILIYOPITA

## 7.1 Utangulizi

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yameendelea kutambuliwa kama wadau muhimu wa maendeleo ya kijamii na kiuchumi, ambapo mchango wao umekuwa ukidhihirika kupitia utoaji wa huduma za kijamii, uwezeshaji wa jamii, uendelezaji wa ujuzi, upatikanaji wa huduma ya elimu, afya msaada wa kisheria, kutokomeza umaskini, uchechemuzi wa masuala ya haki za binadamu, utawala bora, uwazi na uwajibikaji, pamoja na kuchangia uzalishaji wa ajira, mapato ya kodi na fedha za kigeni.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 29(1)(a) na (b) cha Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sura ya 56 ya Sheria za Tanzania, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanatakiwa kuwasilisha taarifa za mwaka za utekelezaji, pamoja na taarifa za fedha zilizokaguliwa. Kupitia uchambuzi wa taarifa hizo, Wizara imekuwa na uwezo wa kubainisha mwenendo wa ufadhili kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa kubainisha kiasi cha fedha kilichopokelewa na kutumiwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika kipindi cha miaka mitano iliyopita.


## 7.2 Mwenendo wa Ufadhili kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yamekuwa yakipokea misaada ya kifedha kutoka ndani (misamaha ya kodi, ruzuku kutoka Serikalini, ada na michango wanachama, mapato ya vitega uchumi, malipo ya huduma, michango ya jamii, wafadhili wa ndani, michango kutoka Sekta Binafsi) na kutoka nje ya nchi (misaada kutoka kwa washirika wa maendeleo wa nje ya nchi). Hata hivyo, kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita, kiasi kikubwa cha fedha za ufadhili kinachopokelewa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kimetoka kwa washirika wa maendeleo wa nje ya nchi.

### 7.2.1 **Vyanzo vya Mapato na Matumizi ya Mashirika**

*Taarifa ya Mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Maendeleo ya Taifa kwa mwaka 2020* iliyotolewa mwezi Septemba 2021, inaonesha kuwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 804 ambayo yalikuwa yanatekeleza shughuli zake Tanzania Bara na ambayo yaliwasilisha taarifa zake kwa usahihi kwenye mfumo, yalipokea kiasi cha Shilingi 1,423,238,932,193 na kutumia kiasi cha Shilingi 1,193,502,074,491 kama inavyoonekana kwenye Umbo 7.2.1.

**Umbo 7.2.1: Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2020**




*Taarifa ya Mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Maendeleo ya Taifa kwa mwaka 2021* iliyotolewa mwezi Septemba 2022, inaonesha kuwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 955 ambayo yalikuwa yanatekeleza shughuli zake Tanzania Bara na ambayo yaliwasilisha taarifa zake kwa usahihi kwenye mfumo, yalipokea kiasi cha Shilingi 1,194,306,453,232 na kutumia kiasi cha Shilingi 1,081,499,948,916 kama inavyoonekana kwenye Jedwali 7.2.1.

**Jedwali 7.2.1: Vyanzo vya Mapato ya Mashirika kwa Mwaka 2021**

| Na. | Aina ya Mapato | Kiasi (Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Bakaa | 20,737,107,780 |
| 2. | Msamaha wa Kodi | 257,949,320 |
| 3. | Ruzuku kutoka Serikalini | 40,600,000 |
| 4. | Ada na Michango ya Wanachama | 8,629,129,324 |
| 5. | Mapato ya Vitega Uchumi | 5,282,542,650 |
| 6. | Malipo ya Huduma | 817,156,221 |
| 7. | Michango ya Jamii | 12,273,273,853 |
| 8. | Wafadhili za Ndani | 11,882,369,268 |
| 9. | Michango kutoka Sekta Binafsi | 2,036,647,563 |
| 10. | Wafadhili wa Nje | 1,132,349,677,253 |
| **Jumla** | | **1,194,306,453,232** |

Vilevile, *Taarifa ya Mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Maendeleo ya Taifa kwa mwaka 2022* iliyotolewa mwezi Oktoba 2023, inaonesha kuwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 1,257 ambayo yalikuwa yanatekeleza shughuli zake Tanzania Bara na ambayo yaliwasilisha taarifa zake kwa usahihi kwenye mfumo, yalipokea kiasi cha Shilingi 2,249,244,846,280 na kutumia kiasi cha Shilingi 2,192,036,989,575 kama inavyoonekana kwenye Jedwali 7.2.2 na Jedwali 7.2.3.

**Jedwali 7.2.2: Vyanzo vya Mapato ya Mashirika kwa Mwaka 2022**

| Na. | Aina ya Mapato | Kiasi (Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Bakaa | 37,183,474,293 |
| 2. | Msamaha wa Kodi | 540,494,949 |
| 3. | Ruzuku kutoka Serikalini | 290,657,498 |
| 4. | Ada na Michango ya Wanachama | 29,230,345,424 |
| 5. | Mapato ya Vitega Uchumi | 3,409,596,633 |
| 6. | Malipo ya Huduma | 5,644,541,839 |
| 7. | Michango ya Jamii | 4,209,588,731 |

| | | |
|---|---|---|
| 8. | Wafadhili za Ndani | 18,776,621,886 |
| 9. | Michango kutoka Sekta Binafsi | 7,582,943,635 |
| 10. | Wafadhili wa Nje | 2,142,376,581,392 |
| **Jumla** | | **2,249,244,846,280** |

**Jedwali 7.2.3: Matumizi ya Fedha za Mashirika kwa Mwaka 2022**

| Na. | Aina ya Matumizi | Kiasi (Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Utekelezaji wa Miradi | 1,959,334,118,380 |
| 2. | Posho na Mishahara | 177,828,623,637 |
| 3. | Kodi ya Uendelezaji wa Ujuzi (SDL) | 2,278,365,128 |
| 4. | Kodi ya Mishahara (PAYE) | 26,120,782,241 |
| 5. | Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) | 25,713,690,118 |
| 6. | Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) | 761,410,071 |
| **Jumla** | | **2,192,036,989,575** |

Aidha, *Taarifa ya Mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Maendeleo ya Taifa kwa mwaka 2023* iliyotolewa mwezi Septemba 2024, inaonesha kuwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 1,368 ambayo yalikuwa yanatekeleza shughuli zake Tanzania Bara na ambayo yaliwasilisha taarifa zake kwa usahihi kwenye mfumo, yalipokea kiasi cha Shilingi 2,614,880,491,980 na kutumia kiasi cha Shilingi 2,461,926,876,419 kama inavyoonekana kwenye Jedwali 7.2.4 na Jedwali 7.2.5.

**Jedwali 7.2.4: Vyanzo vya Mapato ya Mashirika kwa Mwaka 2023**

| Na. | Aina ya Mapato | Kiasi (Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Bakaa | 37,925,158,488 |
| 2. | Msamaha wa Kodi | 271,659,205 |
| 3. | Ruzuku kutoka Serikalini | 3,281,674,634 |
| 4. | Ada na Michango ya Wanachama | 7,013,683,724 |

| | | |
|---|---|---|
| 5. | Mapato ya Vitega Uchumi | 8,355,014,956 |
| 6. | Malipo ya Huduma | 6,954,741,585 |
| 7. | Michango ya Jamii | 3,575,676,963 |
| 8. | Wafadhili za Ndani | 29,939,831,796 |
| 9. | Michango kutoka Sekta Binafsi | 7,130,106,831 |
| 10. | Wafadhili wa Nje | 2,510,432,943,798 |
| **Jumla** | | **2,614,880,491,980** |

**Jedwali 7.2.5: Matumizi ya Fedha za Mashirika kwa Mwaka 2023**

| Na. | Aina ya Matumizi | Kiasi (Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Utekelezaji wa Miradi | 2,139,495,506,090 |
| 2. | Posho na Mishahara | 245,004,730,237 |
| 3. | Kodi ya Uendelezaji wa Ujuzi (SDL) | 2,814,636,314 |
| 4. | Kodi ya Mishahara (PAYE) | 42,598.958,274 |
| 5. | Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) | 30,858,702,827 |
| 6. | Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) | 1,154,342,677 |
| **Jumla** | | **2,461,926,876,419** |

Kadhalika, *Taarifa ya Mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Maendeleo ya Taifa kwa mwaka 2024* iliyotolewa mwezi Julai 2025, inaonesha kuwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 1,360 ambayo yalikuwa yanatekeleza shughuli zake Tanzania Bara na ambayo yaliwasilisha taarifa zake kwa usahihi kwenye mfumo, yalipokea kiasi cha Shilingi 1,449,748,642,857 na kutumia kiasi cha Shilingi 1,289,344,177,596 kama inavyoonekana kwenye Jedwali 7.2.6 na Jedwali 7.2.7.

**Jedwali 7.2.6: Vyanzo vya Mapato ya Mashirika kwa Mwaka 2024**

| Na. | Aina ya Mapato | Kiasi (Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Bakaa | 28,573,425,405 |
| 2. | Msamaha wa Kodi | 72,960,289 |
| 3. | Ruzuku kutoka Serikalini | 1,775,402,079 |
| 4. | Ada na Michango ya Wanachama | 10,990,013,428 |
| 5. | Mapato ya Vitega Uchumi | 12,384,448,084 |
| 6. | Malipo ya Huduma | 1,514,422,348 |
| 7. | Michango ya Jamii | 11,679,208,240 |
| 8. | Wafadhili za Ndani | 13,921,245,183 |
| 9. | Michango kutoka Sekta Binafsi | 6,048,125,018 |
| 10. | Wafadhili wa Nje | 1,362,789,392,783 |
| **Jumla** | | **1,449,748,642,857** |

**Jedwali 7.2.7: Matumizi ya Fedha za Mashirika kwa Mwaka 2024**

| Na. | Aina ya Matumizi | Kiasi (Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Utekelezaji wa Miradi | 980,386,500,732 |
| 2. | Posho na Mishahara | 228,804,362,209 |
| 3. | Kodi ya Uendelezaji wa Ujuzi (SDL) | 2,512,887,034 |
| 4. | Kodi ya Mishahara (PAYE) | 40,244,269,037 |
| 5. | Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) | 32,128,964,990 |
| 6. | Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) | 5,267,193,594 |
| **Jumla** | | **1,289,344,177,596** |

## 7.3 Utekelezaji wa Miradi na Afua Kisekta

Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yalitekeleza miradi na afua mbalimbali. Kwa mwaka 2020, kiasi cha Shilingi 1,422,210,060,455 kilitumika kutekeleza miradi na afua katika sekta ya afya, ulinzi wa jamii, uwezeshaji wa jamii, kilimo, elimu, utawala bora, mazingira, maji, jinsia na haki za binadamu kama inavyoonekana katika Jedwali 7.3.1.

**Jedwali 7.3.1: Utekelezaji wa Miradi kwa Mwaka 2020**

| Na. | Sekta | Kiasi (Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Afya | 578,617,583,288 |
| 2. | Ulinzi wa Jamii | 331,334,064,287 |
| 3. | Uwezeshaji wa Jamii | 245,417,057,839 |
| 4. | Kilimo | 74,847,687,846 |
| 5. | Elimu | 61,711,408,016 |
| 6. | Utawala Bora | 54,430,812,653 |
| 7. | Mazingira | 32,443,097,988 |
| 8. | Maji | 30,619,112,155 |
| 9. | Jinsia | 11,619,112,155 |
| 10. | Haki za Binadamu | 1,159,618,544 |
| **Jumla** | | **1,422,210,060,455** |

Kwa mwaka 2021, kiasi cha Shilingi **942,794,477,792** kilitumika kutekeleza miradi na afua katika sekta ya afya, uwezeshaji wa jamii, ulinzi wa jamii, mazingira, kilimo, elimu, utawala bora, maji, haki za binadamu, jinsia na nishati kama inavyoonekana katika Jedwali 7.3.2.

**Jedwali 7.3.2: Utekelezaji wa Miradi kwa Mwaka 2021**

| Na. | Sekta | Kiasi (Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Afya | 360,810,724,455 |
| 2. | Uwezeshaji wa Jamii | 332,239,023,518 |
| 3. | Ulinzi wa Jamii | 61,478,824,070 |
| 4. | Mazingira | 52,324,452,813 |
| 5. | Kilimo | 47,306,774,582 |
| 6. | Elimu | 44,000,586,605 |
| 7. | Utawala Bora | 18,426,362,089 |
| 8. | Maji | 10,449,181,801 |

| | | |
|---|---|---|
| 9. | Haki za Binadamu | 9,799,297,602 |
| 10. | Jinsia | 4,517,067,410 |
| 11. | Nishati | 1,442,182,847 |
| **Jumla** | | **942,794,477,792** |

Kwa mwaka 2022, kiasi cha Shilingi 1,959,334,118,380 kilitumika kutekeleza miradi na afua katika sekta ya mazingira, afya, ulinzi wa jamii, uwezeshaji wa jamii, elimu, kilimo, utawala bora, maji, haki za binadamu, jinsia, nishati, miundombinu na viwanda kama inavyoonekana katika Jedwali 7.3.3.

**Jedwali 7.3.3: Utekelezaji wa Miradi kwa Mwaka 2022**

| Na. | Sekta | Kiasi (Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Mazingira | 840,692,610,323 |
| 2. | Afya | 533,202,283,282 |
| 3. | Ulinzi wa Jamii | 308,792,900,550 |
| 4. | Uwezeshaji wa Jamii | 120,585,673,782 |
| 5. | Elimu | 63,340,017,559 |
| 6. | Kilimo | 31,749,778,791 |
| 7. | Utawala Bora | 29,830,943,245 |
| 8. | Maji | 11,071,960,862 |
| 9. | Haki za Binadamu | 8,908,075,988 |
| 10. | Jinsia | 8,541,620,194 |
| 11. | Nishati | 2,257,717,848 |
| 12. | Miundombinu | 351,535,956 |
| 13. | Viwanda | 9,000,000 |
| **Jumla** | | **1,959,334,118,380** |

Kwa mwaka 2023, kiasi cha Shilingi 1,208,938,419,590 kilitumika kutekeleza miradi na afua katika sekta ya afya, uwezeshaji wa jamii, ulinzi wa jamii, mazingira, elimu, kilimo, utawala bora, maji, jinsia, haki

za binadamu, nishati na miundombinu kama inavyoonekana katika Jedwali 7.3.4.

**Jedwali 7.3.4: Utekelezaji wa Miradi kwa Mwaka 2023**

| Na. | Sekta | Kiasi (Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Afya | 507,017,325,261 |
| 2. | Uwezeshaji wa Jamii | 281,384,110,075 |
| 3. | Ulinzi wa Jamii | 122,489,218,811 |
| 4. | Mazingira | 98,690,465,665 |
| 5. | Elimu | 79,166,785,015 |
| 6. | Kilimo | 47,977,264,569 |
| 7. | Utawala Bora | 36,287,582,890 |
| 8. | Maji | 12,846,489,968 |
| 9. | Jinsia | 11,505,579,244 |
| 10. | Haki za Binadamu | 10,343,174,647 |
| 11. | Nishati | 772,541,413 |
| 12. | Miundombinu | 457,882,032 |
| **Jumla** | | **1,208,938,419,590** |

Kwa mwaka 2024, kiasi cha Shilingi 980,386,500,732 kilitumika kutekeleza miradi na afua katika sekta ya afya, uwezeshaji wa jamii, ulinzi wa jamii, mazingira, elimu, kilimo, utawala bora, maji, jinsia, haki za binadamu, nishati na miundombinu kama inavyoonekana katika Jedwali 7.3.5.

**Jedwali 7.3.5: Utekelezaji wa Miradi kwa Mwaka 2024**

| Na. | Sekta | Kiasi (Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Uwezeshaji wa Jamii | 370,820,898,559 |
| 2. | Afya | 291,303,490,749 |
| 3. | Mazingira | 80,863,674,279 |
| 4. | Elimu | 76,322,945,446 |
| 5. | Ulinzi wa Jamii | 57,337,725,511 |

| | | |
|---|---|---|
| 6. | Kilimo | 49,846,109,010 |
| 7. | Utawala Bora | 21,633,125,580 |
| 8. | Maji | 12,073,361,551 |
| 9. | Haki za Binadamu | 10,504,562,411 |
| 10. | Jinsia | 8,937,949,113 |
| 11. | Nishati | 539,550,868 |
| 12. | Miundombinu | 199,907,655 |
| 13. | Viwanda | 3,200,000 |
| **Jumla** | | **980,386,500,732** |

## 7.4 Wafadhili wa Miradi na Afua za Mashirika

Katika kipindi cha miaka mitano (5) iliyopita, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yalipokea misaada ya kifedha kutoka kwa wafadhili wa ndani na nje ya nchi ili kufakinisha utekelezaji wa miradi na afua mbalimbali kama inavyoonekana katika Jedwali 7.4.1.

**Jedwali 7.4.1: Wafadhili wa Miradi ya Mashirika Kisekta**

| Na. | Sekta | Wafadhili |
|---|---|---|
| 1. | Afya | Shirika la USAID, Bill & Melinda Gates Foundation, Global Fund, CDC, Mastercard Foundation, Amref Health Africa - Tanzania, KOICA, FCDO, UKAID, PEPFAR, UNICEF, JHPIEGO, MSI Reproductive Choices Tanzania, UNHCR, BPRM, H&B Agerup, Bloomberg Philanthropies, Ubalozi wa Ufaransa, World Vision, National Community Lottery Fund, Washington State University na Pact Tanzania. |
| 2. | Uwezeshaji wa Jamii | Bill & Melinda Gates Foundation, Fintrac, Innovation for Poverty Action, MasterCard Foundation, Policy Forum, Livingstone Tanzania Trust, EU, Nature Friends Dresden, FCS, KOICA, USAID, LSF, GAC, Hans Seidel, NORAD, World Family of Radio Maria, ACN International, Voce Di Maria, Ubalozi wa Sweden, Ubalozi wa Ireland, BOT, Sevde |

| | | |
|---|---|---|
| | | Sevan Usak Vakfi, Convoy of Hope US, DOEN Foundation, Kijana Kwanza UK, UNDP, SwissContact, Girls Foundation US, GN Global Partnership Center, GN Global Impact Foundation, WFP, Friedrich-Ebert-Stiftung, Helvetas Swiss Intercooperation. |
| 3. | Ulinzi wa Jamii | Shirika la USAID, UNHCR, UNICEF, Plan International, NORAD, Abott Fund, WorldShare, EU, WFT, Serikali ya Uingereza, Comfort Aid, PEPFAR, DRC, Rahma International Society, SIDA, Compassion International, RCA, Givewell Foundation, BMZ, GFFO, SOS Denmark, Deloitte Consulting Ltd, FHI360, ISF, UKAID, Liverpool Football Club Foundation na GAC. |
| 4. | Mazingira | Shirika la USAID, FORVAC, SIDA, EU, Jane Goodall Institute, Nature Conservancy, Pams Foundation US, SDC, World Land Trust, Franklyn and Marshal College, The Nature Conservancy, UNDP, Jane Goodhall Institute, AWF, WWF Sweden, WWF UK, WWF Germany, WWF Tanzania, ECA-Tanzania, KopeLion USA, Vi Agroforestry, Frankfurt Zoological Society na NORAD. |
| 5. | Kilimo | EU, NORAD, AGRA, Vi Agro Forestry, USAID, Bread for the World, Bill & Melinda Gates Foundation, Helvetas, Italian Agency Corporation and Development, International Livestock Institute, Laudes Foundation, DGD, Care International (USA), GAC, Ubalozi wa Sweden, Royal Norwegian Society for Development (Norges Vel), KopeLion USA, The Nature Conservancy, FGC, WWF, SIDA, Frankfurt Zoological Society na Rockefeller Philanthropy. |
| 6. | Elimu | Help to Help, Child Fund Korea, Irish AID, UKAID, BMZ, Pestalozzi Children Foundation, Feed the Children, WeWorld Online Foundation (Italy), Helvetas, Segal Family Foundation, UNICEF, SDC, KOICA, KAS, NORAD, SIDA, USAID, GFFO, Room to Read, TFFT USA, Compassion International, World Education Fund USA, GAC, CIC, , Focus on Tanzania Communities (US), GPC, Washington |

| | | |
|---|---|---|
| | | State University, Opportunity Education Foundation, Conrad N. Hilton Foundation, World Learning Ogranization, Malala Fund, Plan International, CAMFED, Village Schools International, GN Global Partership Center na USDA. |
| 7. | Utawala Bora | Shirika la DANIDA, USAID, EU, Ubalozi wa Sweden, Ubalozi wa Norway, FCS, KAS, Fredrick Neuman Howlet Foundation, Ubalozi wa Ireland, Ubalozi wa Denmark, Hempel Foundation, Freedom House, UNA Sweden, African Women Development Fund, Ford foundation, Hewlett foundation, Ubalozi wa Switzerland, SIDA, Global Health Advocacy Incubator (GHAI), Wellspring Philanthropic Fund na Shirika la KAS. |
| 8. | Maji | WorldServe International, Play Smaktir Hayat Derrigi, UNICEF, Life Water International, Stitching SIMAVI, Raleigh International, Comfort Aid International, Charity Water, Water Engineers for the Americas & Africa (WEFTA), Lay Volunteers International Association (LVIA) Italy, German Federal Republic (KFW), Water for People (USA), World Federation (WF-AID) UK, CRS, FCDO, EU, Go Drill Inc na Shirika la Charity Water. |
| 9. | Haki za Binadamu | Shirika la SIDA, EU, We World Online Foundation (Italy), Foundation for Civil Society (FCS), International Work Group for Indegionus Affairs, Legal Services Facility (LSF), Oxfarm GB, T-Marc Tanzania, USAID, Bread for the World, Change Africa Trust, Protection International Africa, Wellspring Foundation, Open Society Policy Centre (OSPC), Global Fund for Women, Segal Family Foundation, TIDES Foundation, Better Way Foundation, Protection International Africa (PIA), Ford Foundation na Rights and Resources Group (RRG). |
| 10. | Jinsia | Shirika la UNFPA, UN Women, Shirika la USAID, FCDO, Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Sweden (SIDA), Shirika la |

| | | |
|---|---|---|
| | | Maendeleo la Canada (GAC), Wizara ya Maendeleo na Ushirikiano wa Kiuchumi ya Ujerumani (BMZ), HelpAge International (Germany), Bread for the World, Children Rights and Violence Prevention Fund, Foundation of Civil Society (FCS), Ubalozi wa Ireland, Project Management Institute Education Fund na Women Fund Tanzania Trust. |

## 7.5 **Hitimisho**

Mwenendo wa ufadhili kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita unaonesha kuwa uhai wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali unakabiliwa na changamoto mbalimbali kutokana na kubadilika kwa masharti na vipaumbele vya ufadhili, mazingira ya kiutendaji na uwezo wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kukabiliana kikamilifu na changamoto zilizopo.

Hata hivyo, idadi kubwa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali imeendelea kutegemea wafadhili hasa wa nje ya nchi, hali ambayo inaweza kuathiri uhai wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali iwapo hakutakuwa na mikakati madhubuti ya kuhakikisha uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali hasa ya ndani.

# SURA YA NANE

# CHANGAMOTO NA MAPENDEKEZO YA KUBORESHA URATIBU WA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI

## 8.1 Utangulizi

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ni wadau muhimu wa maendeleo nchini ambao wamekuwa wakichangia jitihada mbalimbali za Serikali za kuwaletea wananchi maendeleo. Aidha, Mashirika yameendelea kutoa mchango mkubwa kupitia fursa mbalimbali za ajira, pamoja na utekelezaji wa miradi na afua katika sekta za afya, uwezeshaji wa jamii kiuchumi, kilimo, elimu, maji, ulinzi wa jamii, uhifadhi wa mazingira, haki za binadamu, utawala bora na maendeleo ya jinsia.

## 8.2 Changamoto

Kufuatia uchambuzi wa taarifa za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa mwaka 2024, pamoja na majadiliano yaliyofanywa na wawakilishi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali wakati wa zoezi la ufuatiliaji na tathmini ya miradi iliyofanyika katika mikoa yote ya Tanzania Bara, baadhi ya changamoto zilizobainika ni pamoja na:

- Kutowasilisha taarifa kwa mujibu wa Sheria na Kanuni, ambapo kati ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 9,279 yaliyotakiwa kuwasilisha taarifa, ni Mashirika 1,360 tu ndio yaliwasilisha taarifa hizo. Kutowasilisha taarifa hizo kunapunguza utambuzi wa mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Maendeleo ya Taifa.
- Kushindwa kutumia Mfumo wa Kielektroniki wa Usajili na Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NIS) kwa usahihi na hivyo kuwasilisha taarifa ambazo hazijakamilika. Hali hiyo imekuwa ikisababisha kukosekana kwa taarifa sahihi za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na hatimaye kushindwa kabisa kutambua mchango wa Mashirika husika.
- Upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi, ambapo baadhi ya Mashirika yamekuwa yakitekeleza shughuli zao

kwa bajeti finyu. Aidha, vigezo na Masharti ya baadhi ya wafadhili vinakwamisha utekelezaji wa miradi na afua mbalimbali za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

- Ushirikiano hafifu kutoka kwa jamii imebainika kuwa miongoni mwa changamoto zinakwamisha uendelevu wa miradi inayotekelezwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa kuwa baadhi ya makundi katika jamii yanamiini kuwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yamekuwa yakipata fedha nyingi kutoka kwa wafadhili.
- Baadhi ya kodi zinazotozwa kwa Mashirika na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Wakala wa Usalama na Afya Mahala pa Kazi (OSHA) zimetajwa kuwa sio rafiki kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Kwamba, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yamekuwa yakitozwa kodi hizo sawa na zinavyotozwa kwa Makampuni.
- Kukosekana kwa ujuzi mahsusi kwa ajili ya kuyawezesha Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuandaa vyema maandiko ya miradi ya ufadhili (project funding proposals). Kwamba, kukosekana kwa ujuzi mahsusi kumesababisha baadhi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kukosa fursa mbalimbali za ufadhili zinazotolewa na washirika wa maendeleo na sekta binafsi.
- Kusimamishwa kwa ufadhili wa fedha kutoka Serikali ya Marekani, mfano miradi ya afya, kilimo na elimu iliyokuwa inafadhiliwa na Shirika la Misaada la Marekani (USAID).

## 8.3 Mapendekezo

Kwa kuzingatia changamoto mbalimbali zilizobainishwa katika taarifa hii, mapendekezo yafuatayo yametolewa ili kutafuta ufumbuzi wa changamoto zinazoyakabili Mashirika Yasiyo ya Kiserikali hapa nchini na hatimaye kuboresha uratibu na kuongeza ufanisi katika utendaji kazi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali:

- Wizara kupitia Ofisi ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO) kuendelea kuyajengea uwezo Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na wadau mbalimbali kuhusu matumizi ya Mfumo wa

Kielektroniki wa Usajili na Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NIS), sambamba na kuhamasisha uwasilishaji wa taarifa ili kuongeza utambuzi wa mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika nyanja mbalimbali.

- Mashirika Yasiyo ya Kiserikali pamoja na wadau wengine kutumia huduma zinazotolewa na Taasisi ya Usuluhishi wa Malalamiko na Taarifa za Kodi (Tax Ombudsman Service Tanzania - TOST), ambayo ina jukumu la kupitia na kushughulikia malalamiko yote ya walipakodi kuhusu huduma, masuala ya kiutaratibu na kiutawala yanayoweza kujitokeza katika usimamizi wa sheria za kodi kwa usawa na maridhiano.
- Serikali kupitia Wizara, Idara na Taasisi zake kuendelea kujenga, kuimarisha na kuboresha mazingira wezeshi kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na kukua, sambamba na kutoa mafunzo ya mara kwa mara kuhusu Sheria, Kanuni na Miongozo inayosimamia shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.
- Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO) kwa kushirikiana na wadau mbalimbali katika ngazi ya Wilaya, Mkoa na Taifa kuendeleza utaratibu wa kuyajengea uwezo Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika masuala mbalimbali, ikiwemo uandishi wa miradi ya ufadhili na kuweka utaratibu maalum wa kuyaunganisha Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na wafadhili.
- Wizara kupitia Ofisi ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO) kuendelea kuyahamasisha Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya Kimataifa na Mashirika makubwa kuyajengea uwezo Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya ndani na yenye uwezo mdogo kama ilivyoainishwa katika Kifungu cha 31(c) cha Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sura ya 56 ya Sheria za Tanzania.

## 8.4 **Hitimisho**

Taarifa ya Mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Katika Maendeleo ya Taifa kwa Mwaka 2023 Wizara kupitia Ofisi ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali itaendelea kujenga na kuimarisha mazingira wezeshi ya utendaji kazi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili kuongeza utambuzi wa mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika nyanja mbalimbali.

Kwa upande mwingine, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yana jukumu la kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo ya uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi, kuimarisha misingi ya uwazi, uwajibikaji na uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, pamoja na kuongeza utambuzi wa mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika nyanja mbalimbali za maendeleo.

## REJEA


JMT 1996. Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Jamii, 1996. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum.

JMT 1999. Mkakati wa Kitaifa wa Utawala Bora, Ofisi ya Rais, Utawala Bora, Kitengo cha Uratibu.

JMT 2022. Mkakati wa Kitaifa wa Uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 2022/2023 - 2026/2027 (MKIUMA).

JMT 2001. Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, 2001. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum.

JMT 2002. Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sura ya 56 ya mwaka 2002. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum.

JMT 2002. Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake, 2023. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum.

JMT 2013. Mpango wa Kitaifa wa Haki za Binadamu, 2013-2017, Wizara ya Katiba na Sheria.

JMT 2004. Kanuni ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Tangazo la Serikali Na. 152, 2004. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum.

JMT 2020. Mwongozo wa Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Tanzania Bara, 2020. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum.

JMT 1977. Katiba ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, 1977. Wizara ya Katiba na Sheria.

JMT 2003. Sera ya Taifa ya Hifadhi ya Jamii, 2003. Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu

JMT 2014. Sera ya Elimu na Mafunzo, 2014. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.
JMT 2021. Sera ya Taifa ya Mazingira, 2021. Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano na Mazingira.
JMT 2021. Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26. Wizara ya Rais – Mipango na Uwekezaji.
JMT 2013. Sera ya Taifa ya Kilimo, 2013. Wizara ya Kilimo.
JMT 2002. Sera ya Taifa ya Maji, 2002. Wizara ya Maji.
JMT 2007. Sera ya Afya, 2007. Wizara ya Afya




**Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum**

**Mji wa Serikali - Mtumba,**
**Barabara ya Afya,**
**S. L. P 573,**
**40480 DODOMA.**
**Simu Na: 255 (026) 2963341/2963346**
**Nukushi: 255 (026) 2963348**
**Barua Pepe: ps@jamii.go.tz**
**Tovuti: www.jamii.go.tz**